UKURASA WA 3
**Nawanda** afunguka magumu aliyopitia katika kesi ulawiti

UKURASA WA 3
**Bodaboda**, mwenzake wapandishwa kizimbani mashtaka ya kumuua mtoto, warudi rumande

**Mzigo** wa kihistoria dawa za kulevya visiwani wanaswa, ungezalisha kete milioni 27 UKURASA WA 17

24/25


# Nipashe

Jumanne Desemba 31, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581908

www.ippmedia.com

Nipashe Digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710

LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


## KWAHERI 2024...

# Dk. Mwinyi aorodhesha yanayoing'arisha Z'bar

UK.2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akitoa salamu za Mwaka Mpya.

UKURASA WA 8

## WAMTAKIA SAMIA HERI KWA UONGOZI WENYE UADILIFU

## Askofu aibuka tena kunusuru mpasuko ndani ya CHADEMA

UKURASA 15

## RIPOTI MAALUM

# Selimundu inavyowatesa wagonjwa na wazazi wao



• **Kila** mwaka wanazaliwa 14,000 wenye shida hiyo *Endelea Ukurasa 4&5*

**MICHEZO** **RAMOVIC APAGAWA VIWANGO YANGA SC** UK.24

**MAONI,** UK.6

KWAHERI 2024...

# Dk. Mwinyi aorodhesha yanayoing'arisha Z'bar

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameelezea mafanikio ya serikali yake katika kipindi cha mwaka 2024 ikiwamo kukuza uchumi kwa kuongeza udhibiti na ukusanyaji wa mapato.

Rais Mwinyi ameweka hayo bayana katika risala yake za kuuaga mwaka 2024 na kuukaribisha mwaka 2025.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuimarisha uwekezaji na biashara, ujenzi wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini, viwanja vya ndege na bandari, ujenzi wa nyumba za makaazi, usambazaji wa huduma za umeme na majisafi na salama pamoja na uimarishaji wa sekta ya elimu na afya kote nchini.

Kadhalika, alisema serikali yake imefanikiwa kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuanzisha programu za utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa makundi ya wananchi na kuwajengea mazingira bora ya kufanya biashara hasa baada ya kufunguliwa rasmi kwa masoko makubwa ya kisasa ya Mwanakwerekwe na Jumbi.

Pia, ameeleza mafanikio aliyoyapata kupitia sekta ya michezo na kwamba tayari serikali yake inakamilisha mwaka 2024 ikiwa imepiga hatua kubwa katika kuimarisha sekta ya michezo kwa mafanikio baada ya kufanya ukarabati mkubwa wa viwanja vya michezo vya Amani Complex, Gombani, sambamba na ujenzi wa viwanja vya michezo mbalimbali pamoja na hoteli ya Amani.

"Jitihada hizi zinalenga kuzidi kuimarisha sekta ya michezo na kuchochea shughuli za utalii kupitia michezo na matamasha. Aidha, tumedhamiria kuwa na miundombinu ya michezo yenye kukidhi mahitaji ya mashindano ya CHAN mwaka 2025 na ya Afcon mwaka 2027 yatakayoandaliwa kwa pamoja kati ya Tanzania, Kenya na Uganda," alisema Rais Mwinyi.

"Tuna wajibu mkubwa wa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa katika nchi yetu na kutokana na misingi hiyo, nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika jitihada zetu za kukuza uchumi, kuimarisha miundombinu, biashara na uwekezaji, huduma za jamii na kuimarisha demokrasia na utawala bora."

Rais Mwinyi alisema mafanikio mengine yaliyopatikana katika mwaka 2024, yataelezwa na mawaziri wake.

**RAI KWA WAFANYAKAZI**

Alitoa rai kwa wafanyakazi wote kuongeza kasi ya kufanya kazi kwa bidii zaidi kwa mwaka ujao kila mtu kwa nafasi yake katika kufanikisha jitihada za kujiletea maendeleo.

**UCHAGUZI MKUU**

Rais Mwinyi alisema tayari serikali zote mbili; Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Tume za Uchaguzi, NEC na ZEC



zimeanza kuchukua hatua za matayarisho kuhakikisha nchi inaendesha uchaguzi kwa misingi ya haki na sheria.

Alitaka wananchi kuendelea kudumisha amani kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

"Ni wajibu wa viongozi wa kisiasa, taasisi za kijamii, viongozi wa dini, na wananchi wote kukumbushana umuhimu wa kudumisha na kuilinda amani tuliyonayo ili tuzidi kupiga hatua za maendeleo kwa faida ya kizazi cha sasa na wale watakao kuja baada yetu.

"Tunapoukamilisha mwaka huu wa 2024, navishukuru sana na kuvipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na amani kwa wananchi pamoja na wageni wanaoitembelea nchi yetu," alisema Rais Mwinyi.

**AHADI 2025**

Rais Mwinyi alisema serikali yake itaendelea kuhakikisha amani iliyopo inaendelea kudumu na kuahidi kuongeza kasi ya utekelezaji maendeleo.

"Niwaombe wananchi waendelee kuipa serikali ushirikiano hasa kwa kudumisha amani, umoja na mshikamano ili kwa pamoja kupiga hatua za maendeleo tunayoyatarajia. Nachukua fursa hii kutoa salamu za mwaka mpya kwa wananchi wote wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa salamu kwa viongozi wa serikali na nchi rafiki, taasisi za kimataifa na washirika wetu wote wa maendeleo."

**SHEREHE YA MIAKA 61 YA MAPINDUZI**

Akizungumzia sherehe za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais Mwinyi alisema tayari shughuli mbalimbali za maadhimisho ya sherehe hizo zimeshaanza tangu 15 Desemba kwa usafi wa mazingira katika maeneo mengi ya nchi.

Alitoa wito kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi katika matukio mbalimbali yaliyoandaliwa kwa ajili ya sherehe hizo ikiwa ni hatua ya kuonesha uzalendo na kuthamini jitihada za waasisi za kufanya Mapinduzi ili kuikomboa nchi.

"Matukio hayo yanajumuisha uzinduzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na uwekaji wa mawe ya msingi, shughuli za michezo na utamaduni na yatafikia kilele chake Januari 12 katika uwanja wa Gombani Pemba," alisema Rais Mwinyi.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Lema aibuka na hoja nyingine, CHADEMA yasema haitekelezeki

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimejibu hoja iliyotolewa na Mwenyekiti mstaafu wa chama hicho Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema kuhusu uteuzi wa mgombea wa nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu ujao.

Kupitia akaunti yake ya X, Lema alipendekeza jana kuwa Mkutano Mkuu wa chama hicho utakaofanyika mwezi unaonza kesho, utoke na jina la mgombea urais.

Lema pia alipendekeza mkutano utoe mamlaka kwa Kamati Kuu au Baraza Kuu la chama hicho kutafuta mgombea mwenza na kumthibitisha kwa niaba ya mkutano mkuu ili chama kitoke na jina la mgombea sambamba na viongozi wakuu wa chama hicho.

"Ingewezekana Mkutano Mkuu wa chama chetu utakaofanyika Januari, utoke na jina la mgombea urais na pia utoe mamlaka kwa Kamati Kuu/Baraza Kuu kutafuta mgombea mwenza na kumthibitisha kwa niaba ya Mkutano Mkuu ili chama kitoke na jina la mgombea sambamba na viongozi wakuu wa chama.

"Jambo hili ni muhimu kwa ajili ya 'branding' (kumtangaza kwa lengo kuongeza umaarufu) ya mgombea urais na masuala ya uratibu wa masuala ya kampeni na rasilimali fedha kwa mgombea.

"Pengine wazo hili likifanyiwa kazi, bila shaka tunaweza kumaliza salama zaidi na kupunguza kelele nyingi zisizokuwa na maana. Kamati Kuu inaweza kufikiri hivi," aliandika Lema.

Nipashe iliwasiliana na uongozi wa CHADEMA kuzungumzia hoja hiyo ya Lema, ukiwa na majibu kwamba hoja hiyo haitekelezeki kwa kuwa muda uliobaki kufikia Mkutano Mkuu wa chama ni mfupi.

"Ni maoni na ushauri wake kama mwanachama, yatapimwa kwa kuzingatia uzito wa hoja husika kwa wakati mwafaka," alisema John Mrema, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA.

Mrema alimweleza zaidi mwandishi wa Nipashe, akisema: "Kuhusu utaratibu wa kumteua mgombea urais, Katiba yetu imeweka utaratibu. Ibara ya 7.7.16, kazi za Kamati Kuu ni kufanya utafiti wa wagombea urais na mgombea mwenza na kuwasilisha ripoti zake kwa Baraza Kuu la chama.

"Hivyo, kwa mujibu wa ibara tajwa hapo juu, ni wazi kuwa wazo lake halitekelezeki kwa huu muda mfupi ambao tumebakiwa nao kabla ya Mkutano Mkuu wa chama kufanyika."

IN THE DISTRICT COURT OF NYAMAGANA DISTRICT AT MWANZA
CIVIL/ CRIMINAI APPEAL NO: 6373 OF 2024
BANK OF AFRICA (T) LTD PLAINTIFF/APPELLANT
VERSUS
JAGILI MGANGA KADASO
DEFFENDANT/RESPONDENT

NOTICE OF DATE OF JUDGEMENT

**TAKE NOTICE THAT** the above case has been fired for Judgment on the 24 day of **JANUARY, 2025 at 8:30 a.m**. before **Hon. SUMARI SEM** in the forenoon.
**YOU ARE** required to appear before this court without fail and you must produce all documents upon which you intend to rely in support of your case.
**GIVEN UNDER** my hand and the SEAL of the court this 04 day of DECEMBER, 2024

**TO BE SERVE UPON:**
- **JAGILI MGANGA KADASO**

SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE MWANZA

KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**DEBORA MATHIAS KAAYA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 861 CFG** . Chassis No. **MD2A21BY5YKWM87648** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DAR/UBU/290004/2024**

MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM
Shauri la Madai/Ndoa Na. 1723 / 2024
Jina la Mdai: PASCAL ANDREW MAYALLA
Jina la Mdaiwa: JOYCE ABEL MMARI
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

**Kwa: JOYCE ABEL MMARI**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) TALAKA – HUKUMU**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 31 Mwezi 12 Mwaka 2024 saa 4:00 asubuhi. Mbele ya Mh. MWAGENI kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri ya Muhuri wa Mahakama hii leto tarehe 10 Mwezi 12 Mwaka 2024

HAKIMU

KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ZAMDAT MATHIAS SHUMBUSHO** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba **TAE 170134** iliyotolewa uhamiaji makao makuu tarehe **23 AUGUST, 2019.** Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi:**PHQ/DAR/ILA/200943/2024**

KUPOTEA KWA CHETI



**KIDAHA MOHAMED SALUM** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha sita chenye Index No. **S0109-0648** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IHUNGO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2012.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi**: PHQ/DAR/TEM/150001/2024**

## Wawili wapandishwa kizimbani kwa mashtaka kumuua mtoto Greyson

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU wawili wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma kwa mashtaka ya kumuua kwa kukusudia mtoto Greyson Kanyenye (6) katika mtaa wa Ilazo, jijini Dodoma Desemba 25 mwaka huu.

Hao ni Kelvin Joshua (27) na Tumaini Msangi (28) ambao wote walisomewa mashtaka yanayowakabili na Wakili Mwandamizi wa Serikali Patricia Mkina mbele ya Hakimu Mkazi Denis Mpelembwa.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili Mkina alidai washtakiwa wote wawili walifanya kosa la mauaji ya Greyson Kanyenye, Desemba 25, mwaka huu kinyume cha vifungu namba 196 na 197 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Hakimu Mpelembwa alisema mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza mashauri ya mauaji, hivyo washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote mahakamani huko.

"Kosa la mauaji halina dhamana, hivyo mtarudi mahabusu hadi kesi yenu itakapotajwa tena Januari 13, 2025," alisema Hakimu Mpelembwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, akizungumzia tukio hilo Desemba 25 mwaka huu, alisema mwili wa mtoto huyo ulikutwa ndani ya nyumba ukiwa na majeraha shingoni.

Kamanda Katabazi alisema tukio hilo lilitokea saa moja asubuhi katika mtaa wa Bwawani, Ilazo Extension, jijini Dodoma, nyumbani kwa Ofisa Uvuvi wa Mtera, Hamis Mohamed.

Alisema kuwa siku hiyo, Hamis na mama wa mtoto Greyson walikuwa wametoka nyumbani kwa ajili ya matembezi, wakimwacha mtoto huyo chini ya usimamizi wa dereva bodaboda Kelvin.

Alidai kuwa bodaboda huyo alifahamika kwa familia ya mtoto huyo kupitia huduma ya usafiri anayotoa kwa familia yao.

"Bodaboda huyo aliachiwa mtoto ili amwangalie kipindi ambacho watakuwa kwenye matembezi, wawili hao wakati wa usiku waliporudi, mtoto hawakumwona hadi asubuhi majira ya saa moja walipomkuta katika chumba akiwa ameuawa, mwili ukiwa na alama za kupigwa na kitu kizito shingoni mwake," alisema.

Kamanda Katabazi alisema Jeshi la Polisi lilimshikilia bodaboda huyo kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa tukio hilo la mauaji huku akitoa wito kwa wazazi kuacha tabia ya kukabidhi watoto wao kwa watu ambao hawawajui vizuri ili kuepusha matukio kama hayo.

## Nawanda afunguka magumu aliyopitia katika kesi ya ulawiti

**Na Vitus Audax**

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda amezungumza kwa mara nyingine baada ya kushinda kesi ya ulawiti, akisimulia magumu aliyopitia kipindi chote cha kesi hiyo.

Dk. Nawanda alieleza hayo juzi wakati wa misa ya kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan na kumkumbuka baba mzazi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa iliyofanyika katika mtaa wa Nyakabindi, mjini Bariadi.

Alisema kuwa kipindi cha kesi yake kilimfundisha thamani ya kuishi vizuri na watu, akitoa shukrani kwa wananchi wa Simiyu kwa madai walionesha mapenzi makubwa na walimwombea kwa bidii.

"Niwashukuru wananchi kwa dua na maombi yenu ambayo mlikuwa mkiniombea wakati ninapitia kipindi kigumu sana ambacho pia nilihitaji uwapo wa Mungu. Kwa hakika Mungu anampa mtihani mtu anayempenda," alisema Dk. Nawanda.

Alisema kuwa wakati wowote Mungu hawezi kumpa mtihani mja wake ambao hawezi kuuhimili na kuwa alipewa mtihani huo akijua kuwa atauhimili.

"Pia alijua nina watu na watu ndiyo ninyi. Kwahiyo jamani ninawashukuru sana kwa dua zenu. Ninawashukuru kwa kila kitu," alisema Dk. Nawanda.

Aliwashauri viongozi kuishi vizuri na watu na kwa ukaribu kwa kuwa hakuna anayetambua kesho yake. Alisema ukaribu huo ni watu ni mtaji mkubwa katika maisha yake.

"Mwaka jana nilikuja hapa kama mkuu wenu wa mkoa lakini mwaka huu nimekuja kama Nawanda tu wa kawaida. Kwahiyo Simalenga (Mkuu wa Wilaya ya Bariadi) haya maisha yanabadilika sana," alisema Dk. Nawanda.

Alisema kuwa sasa ameamua kuwekeza nguvu zake Newala na kuwa anapambana kwa ajili ya eneo hilo, akitaja kuwa na jambo lake aliloliacha katika kile alichokiita "mabano na litajulikana rasmi 2025".

"Hata hivyo, hili jambo langu la Newala limeishaisha, hivyo msiniulize ni jambo gani, nitawaambia mwakani na wakati utakapofika 2025," alisema Dk. Nawanda.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa alisema ni muhimu kumwombea Rais Samia kutokana na kazi anayofanya katika kuletea taifa maendeleo.

Novemba 20 mwaka huu, Dk. Nawanda aliachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mwanza baada ya kutomkuta na hatia katika kesi ya kulawiti iliyokuwa inamkabili.

Dk. Nawanda alipandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza Julai 9, 2024 na kusomewa shtaka moja la kulawiti kinyume cha kifungu namba 154 (1) (a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, SURA 16, kosa alilodaiwa kutenda Juni 2, 2024.

Alidaiwa kumlawiti mwanafunzi wa chuo kimoja mkoani Mwanza katika eneo la maegesho ya magari lililoko Rock City Mall, wilayani Ilemela mkoani hapa.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 31/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MARGRETH MTEI MWAISAKA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MAGRETH MTEI MWAISAKA NA MASHAKA MWAISAKA | KIMARA | 19/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | RAPHAEL BONIVENTURE MMANDA | NYUMBA | BENEDICT MWITA ROBERT | IGOMA - MWANZA | 10/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | NEW FATHER BOLT GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | ABDALLAH SULTANI MATOPE | MBAGALA CHARAMBE | 11/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | KALINDAGA GENERAL SUPPLIES LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.DSMT1005181,KIWANJA NA. P6772 2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.DSMT1024170,KIWANJA NA. P30034 | 1.SAMWEL THEODOSIA KABETA 2. ERNEST JEROME KALINDAGA | 1.GOBA 2.KIMARA | 18/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | PRAYGOD JUDICA MUSHI | NYUMBA (2) | 1.PRAYGOD JUDICA MUSHI 2.CHRISTINA JOEL PANJA | 1.MWANDEGE 2. MBWENI | 19/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | CONJESTA AMOSI MBILINYI | NYUMBA YENYE HATI NA. 66379 KIWANJA NA.77, KITALU " 22" | DONALD DAVID MATEBELE | BUNJU | 19/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ELIAKIMU KWACHA OMOLO | 1.NYUMBA YENYE HATI NA.79041,KIWANJA NA. 412 2.NYUMBA YENYE HATI NA.95645 | 1.CHARLES MWITA CHACHA 2.ELIAKIMU KWACHA OMOLO | 1.KANGAYE MWANZA 2. MBUGANI MWANZA | 18/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | DAUMU NURSERY AND PRIMARY SCHOOL | NYUMBA | MWINYIHATIBU SALIM MUSTAFA | KIMWANI-CHANIKA | 20/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MAGDALENA GASPER MUSHY | NYUMBA | BEATRICE MUJUNI MWIJAGE | MBEZI-MSINGWA | 19/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 20/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HAPPINESS NYANDA MAYALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SAIDI NYANDA MAYALA | IGOMA MWANZA | 18/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MAGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA (3) VYENYE HATI MILIKI | MAGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 20/01/2025 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0784717164/0714939933/0759648448/0715868000/0714208208/0759648448/0755337777/0715363537/0713306054**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

RIPOTI MAALUMU



# Selimundu inavyowatesa wagonjwa, wazazi wao

Na Sanula Athanas

UNAPOTAJA ugonjwa selimundu, tafsiri ya awali inayobeba picha halisi ni mateso kimwili, kiuchumi na kijamii.

Kuna safari zisizoisha hospitalini, kulala wodini, mahitaji ya kuongezwa damu mara kwa mara, huku upande wa pili ukiakisi gharama kwa anayemhudumia mgonjwa.

Hali iliyopo, sehemu kubwa ya wanaougua na kuuguza, uelewa wao kuhusu maradhi hayo ni mdogo; mara nyingi huufahamu undani wake pindi wanapokuwa katika pilika za matibabu. Vilevile, vituo vya tiba ngazi ya chini, katika itifaki ya utendaji havina mamlaka ya kutibu shida hiyo.

Kuna cha simanzi zaidi, serikali inakiri nusu ya wanaozaliwa na selimundu hufariki dunia ndani ya miaka mitano ya kuzaliwa kwao.

Ili kukabili ugonjwa huo, serikali italazimika kutenga Sh. bilioni 770 kutibu zaidi ya watoto 14,000 wanaozaliwa na maradhi hayo nchini kila mwaka.

Lakini haya yote yanaweza kuepukika ikiwa serikali itatoa elimu kwa wananchi kuhusu ugonjwa huu au kutunga sheria ya kuzuia wananchi kuoana pasi na kupimwa selimundu.

Wataalamu wa selimundu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam, Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando jijini Mwanza na Hospitali ya Rufani ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma wamezungumza kwa kina na Nipashe kuhusu ugonjwa huu, hata kutoa ushauri huo kwa serikali.

Kutibu selimundu ni kupandikiza uloto. Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, gharama ya matibabu hayo nchini inaanzia Sh. milioni 50 hadi 55 kwa kila mgonjwa. Upandikizaji uloto nchini kwa sasa unafanywa BMH kwa gharama za serikali.

Kwa watoto 14,000 wanaozaliwa na tatizo hili, maana yake serikali italazimika kutenga zaidi ya Sh. bilioni 770 kwa ajili ya matibabu ya watoto hao kila mwaka.

Daktari Bigwa wa Magojwa ya Watoto na Mtaalamu wa Selimundu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Emmanuela Ambrose, anasema tatizo la ugonjwa huo ni kubwa nchini.

Bingwa huyo anasema utafiti unaonesha asilimia 75 ya watoto wanaozaliwa na ugonjwa wa selimundu duniani wanatoka Afrika. Tanzania ni nchi ya nne duniani na ya tatu Afrika kwa tatizo hilo. Wengi wao wanatoka Ukanda wa Ziwa Victoria.

Dk. Emmanuela anasema Bugando hivi sasa ina zaidi ya watoto 1,000 wenye shida ya selimundu wanaohudhuria kliniki kwa mwaka. Kila Jumatatu wanawaona watoto 30 hadi 50, huku Ijumaa wakiwaona watoto 50 hadi 80.

"Tunatoa ushauri na kuwaelimisha wazazi na walezi kuwa ugonjwa wa sikoseli hurithiwa kutoka kwa wazazi wote wawili; baba na mama. Pia tunatoa elimu jinsi ya kuepuka kupata mtoto mwenye tatizo hili.

"Watoto wengi wanazaliwa wakiwa na shida hii. Tatizo hili ni kubwa kwa sasa kutokana na watu kutokuelewa wamerithi chembechembe za ugonjwa huu, wanatambua tu pale wanapopata mtoto mwenye shida hii.

"Kusubiri mpaka upate mtoto ni kuchelewa, wanapaswa watambue hali zao kabla ya kubeba ujauzito. Kama wote wana urithi wa selimundu, wafanye uamuzi mapema. Hivyo ni vyema wakapima kabla ya kuingia katika ndoa," Dk. Emmanuela anasema.

Bingwa huyo anashauri mtoto akishazaliwa tu apimwe. Akibainika ana tatizo hilo, aanzishiwe kliniki na matibabu ya selimundu mapema ambayo yatamsaidia kutibu matatizo yote yanayotokana na ugonjwa huo, hata kumfanya aishi muda mrefu.

Njia nyingine ya kukabiliana na ugonjwa huo, Dk. Emmanuela anashauri mama mjamzito anapoanza kliniki apimwe hali yake.

"Kama akibainika amebeba chembechembe za selimundu, iandikwe kwenye kadi yake ya kliniki "AS" (ana chembechembe za selimundu), iandikwe "SS" kama ana selimundu au "AA" kama hana chembechembe wala selimundu.

"Watoto wote watakaozaliwa na mama mwenye "SS" au "AS", lazima wapimwe hali zao watakapozaliwa. Hiyo itasaidia kuondokana na ugonjwa huu," Dk. Emmanuela anashauri.

Bingwa huyo pia anashauri shuleni kuwe na somo mahususi la selimundu kuchochea jitihada za kukabili ugonjwa huo na upimaji selimundu ufanyike hadi shuleni ili watoto wajue hali zao wakiwa wadogo, akiamini hatua hiyo itawasaidia kutambua hatari iliyoko mbele yao na watakuwa makini.

Dk. Emmanuela ana angalizo kwa jamii, akisisitiza kuwa matibabu ya selimundu ni ghali. Ni ugonjwa wa kudumu. Mzazi lazima awe na fedha.

Kuhusu matibabu ya selimundu, Bingwa wa Magonjwa ya Watoto MNH, Dk. Evance Godfrey, anafafanua kuwa mtoto akigundulika ana ugonjwa huo, anaanzishiwa dozi ya Folic Acid inayosaidia uzalishaji damu.

"Pia anaanzishiwa dozi nyingine ya Penicillin V inayozuia magonjwa yanayosababisha vifo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na anapofikisha umri wa miezi tisa anaanza dozi ya Hydroxyurea," Dk. Godrefy anafafanua.

Katika hilo la matibabu, bingwa mwenzake Dk. Emmanuela anatamani serikali isaidie kutoa dawa kwa wagonjwa wa selimundu, hasa dozi ya Hydroxyurea inayosaidia kupunguza shida zinazotokana na selimundu yakiwamo maumivu ya viungo, kulazwa hospitalini na kuongezwa damu mara kwa mara, kuzuia kupata kiharusi (kupooza) na damu kuwa nyepesi.

"Kupandikiza uloto ndiyo tiba ya selimundu, lakini ni gharama sana. Pia lazima uloto huo ni lazima utoke kwa ndugu yako unayeendana naye kibaiolojia (vinasaba). Hapa nchini ni watoto wanane tu wamefanyiwa upandikizaji na wote wako salama, lakini nina imani wengi zaidi watafanyiwa, hasa ambao Hydroxyurea haijawa msaada kwao," anafafanua.

**KULIKONI KANDA YA ZIWA?**

Dk. Emmanuela anasema Kanda ya Ziwa ni moja ya kanda za kitropiki ambazo zina tatizo kubwa la malaria, akiwa na ufafanuzi kwamba mwili wa binadamu umeshabuni njia ya kupambana na malaria kwa kusababisha hitilafu katika vinasaba na kuleta urithi wa selimundu.

"Kwa hitilafu hii warithi waliweza kuishi kwa kujikinga na ugonjwa wa malaria uliokuwa chanzo kikubwa cha vifo. Hitilafu hiyo ikirithiwa kutoka kwa wazazi wote wawili, ndiyo huleta ugonjwa wa selimundu.

"Kuoana wenyewe kwa wenyewe katika ukanda huu wa kitropiki linaonekana jambo la kawaida, lakini ni chanzo cha ongezeko la ukubwa wa tatizo la selimundu Kanda ya Ziwa.

"Kitu cha muhimu ni kufanya vipimo kabla ya kuoana na ikibainika mna urithi wa selimundu, bora msioane ili kuepuka kupata mtoto mwenye ugonjwa huu," anasema Dk. Emmanuela na kushauri kwamba, "ikiwezekana kuwe na sheria inayolazimisha wananchi kupima selimundu kabla ya kuoana.

Hoja ya kuepuka kuoana wenye urithi wa selimundu, inaungwa mkono na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Kansa kwa Watoto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Shakilu Jumanne, anayesema kuwa licha ya mikakati mingi ya kupunguza makali ya ugonjwa huo, hali ni mbaya nchini.

Dk. Jumanne anasema watoto wengi wanaendelea kuteseka na ugonjwa huo kutokana na uelewa mdogo wa wazazi kuhusu namna ya kuepuka mazingira yanayoweza kuchochea seli nyekundu kubadilika umbo na kuwa mundu.

Kama ilivyotolewa angalizo na mtangulizi wake Dk. Emmanuela, Bingwa Jumanne anashauri watu wenye vinasaba vya ugonjwa huo wasioane.

"Kila mwaka nchini, zaidi ya watoto 14,000 huzaliwa na ugonjwa huu. Kati yao, 10,000 huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa. Mwanza pekee wanazaliwa zaidi ya watoto 1,700 kila mwaka wenye tatizo hili," Dk. Jumanne anabainisha.

Kwa lugha rahisi ya hisabati, takwimu hizo zina maana kwamba, kila siku watoto 39 wanazaliwa wakiwa na ugonjwa wa selimundu nchini. Kati yao, 28 (asilimia 72) huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa huku Mwanza pekee ikiwa na wastani wa watoto watano kwa siku.

Kuhusu matibabu ya ugonjwa huo, Dk. Jummanne anaungana na Dk. Emmanuela kwamba njia ya uhakika zaidi ni kupandikiza uloto kutoka kwa ndugu wa karibu kwenda kwa mtoto mwenye tatizo.

"Matibabu ya selimundu ni ghali, hususani katika kupandikiza uloto. Hivyo, ili kuepuka haya, lazima jamii ikubaliane kupima kabla ya ndoa ili kuwaepusha watoto wetu na maumivu wanayopitia watoto wenzao wenye maradhi ya selimundu," bingwa huyo anashauri.

**MIKASA MITAANI**

Isivyo bahati, wote walio mifano ya kujifunza ni kinamama walimu, maradhi ya selimundu yamewatia misukosuko kwa watoto wao.

Mwalimu Hollo Lumala (33), miaka 12 iliyopita alibahatika kupata mtoto wa kike, lakini mikasa ya selimundu ilimpokonya kichanga hicho.

Kwa ufupi, alijifungua mwezi Desemba 2012 na maisha ya malezi yalikuwa shwari hadi Julai 29, 2013, ghafla mtoto alipata homa kali, kidole mkononi kikavimba na alipofikishwa katika zahanati ya Masengwa, wilayani Shinyanga, akapewa maelekezo ya tahadhari ku-

Inaendelea Ukurasa 5

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Selimundu inavyowatesa wagonjwa, wazazi wao

Inatoka ukurasa 4

hadhari kutoka kwa tabibu "huyu mtoto anaonekana ana upungufu wa damu, mpelekeni hospitali kubwa".

Alipofikishwa katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga siku hiyo hiyo, ikathibitishwa ni shida ya upungufu wa damu, lakini wakati wa mchakato kumwongeza damu, mtoto alipoteza maisha akiwa na miezi saba tu duniani.

Mnamo Julai ya mwaka uliofuta, akiwa mkoani Dar es Salaam yaliko makazi yake, alijifungua mtoto wa kike baada ya kupitia mchakato wa uzazi ndani ya mwaka huo mmoja; mtoto akiwa salama kiafya hadi sasa.

Januari ya mwaka huu unaoisha leo, alibahatika kupata mtoto wa kiume. Safari hii mkasa ulianzia alikozaliwa hospitalini Kairuki, akagundulika ana manjano, hata ikamweka wodini kwa siku saba.

Mwalimu Hollo anasimulia maendeleo ya afya baada ya hapo yalikuwa mazuri hadi Julai mtoto alipogundulika kuvimba kidole cha mkono wa kulia. Aliwahishwa katika zahanati jirani alikopata huduma ya sindano ya kutoa sumu, ikihisiwa alikuwa ameng'atwa na mdudu.

Anasimulia kuwa baada ya siku tatu, kidole kingine cha mkono tofauti kilivimba. Mtoto akapelekwa katika Hospitali ya Kairuki, ambako huduma za kibingwa zikabaini ana selimundu.

Mwalimu Hollo anaeleza kuwa hatua ya kwanza ya tiba ilikuwa ni kukabili athari zinginezo, huku akiongezwa damu chupa moja, ikiendana na kuanzishiwa dozi ya tiba ya selimundu kwa mtoto mwenye umri wa chini ya miezi tisa.

Mwezi uliofuata, huku mtoto huyo akianza kuota meno, mama yake anasimulia aliona tena dalili za upungufu wa damu kwa mwanawe ambazo alikuwa ameshafundishwa hospitalini, hata akamrejesha alikotibiwa. Huko ikathibitishwa tena ana upungufu wa damu na akaongezwa, ikiendana na dawa.

Anasimulia kuwa mwezi Septemba alisafiri na mwanawe kwenda mkoani Shinyanga, mtoto akapatwa na dalili za awali, safari hii akalazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga kwa siku mbili, akiongezwa damu.

Kufika Novemba, Mwalimu Hollo anasimulia mkasa ukamrejea tena mwanawe, wakiwa Dar es Salaam, hata wakalazimika kufunga safari ya saa saba usiku kwenda Muhimbili ambako mtoto alipokewa na kulazwa kwa siku nne, akiongezwa damu chupa mbili.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, safari hii tiba iliendana na kuanzishiwa rasmi dozi ya Hydroxyurea inayozuia uwezekano wa maradhi mengineyo kama vile kiharusi, damu kuwa nyepesi na maumivu ya viungo yasiyokoma.

Mwalimu wa pili, Aman Stanslaus (37), mkazi wa Busega mkoani Simiyu, ukimwangalia kiumri na nyakati alizopitia, anashabihiana na mtangulizi wake, wote wakiangukia taaluma moja.

Miaka 10 iliyopita, alipoteza wanawe wawili kutokana na selimundu huku akitengana na mumewe. Katika miaka minne ya mwanzo ya ndoa na mwalimu mwenzake (jina tunalihifadhi), walipata mtoto.

Ilipotimu mwaka 2018, kukaripotiwa malalamiko ya mtoto wao anasumbuliwa na maumivu ya viungo vya mwili, wakati mtoto huyo akisoma shule ya bweni na



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel

kuanza matibabu.

Mwalimu Aman anawasilisha simulizi hiyo kwa sauti ya chini, inayobeba tafsiri ya simanzi, akiwa na ufafanuzi kwamba: "Baada ya vipimo katika Hospitali ya Wilaya ya Magu, madaktari walituambia kuwa mwanangu anasumbuliwa na homa.

"Baada ya muda akawa ameishiwa damu, wakamwongeza. Tukaruhusiwa kurejea nyumbani, lakini baadaye akaishiwa damu tena, ndipo madaktari wa hospitali hiyo walipojiuliza 'kwanini anaishiwa damu kwa muda mfupi baada ya kuongezwa?'

"Wakalazimika kumpima sikoseli (selimundu) na majibu yalipotoka alibainika kuwa 'positive' (taarifa chanya, yaani alikuwa na ugonjwa huo).

"Sikuwa na uelewa wa ugonjwa huu, lakini mtoto alianza kupatiwa matibabu na alirejea shuleni. Ghafla hali ilibadilika na kuishiwa damu."

Mwalimu Aman anataja ndiyo ukawa mwanzo wa kutokuelewana ndani ya familia, kila mmoja akimtupia lawama mwenzake kuwa chanzo cha tatizo. Baadaye lawama zote zilielekezwa kwake

"Hapo ndipo matibabu yakahamia kwenye miti shamba, lakini mimi sikuwa na mrengo huo. Mume wangu na familia yake walijikita katika imani hiyo. Mimi nikajikita katika huduma za hospitalini ingawa kuna wakati walimleta mganga wa kienyeji nyumbani kwa ajili ya kutoa huduma kwa mtoto," anasimulia.

Anasema kuwa wakati wanaendelea na matibabu ya mtoto huyo, alijifungua mtoto mwingine. Naye akawa na selimundu. Wakamwanzishia kliniki ya matibabu ya ugonjwa huo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando.

"Baadaye nikapata mimba nyingine ya mtoto wa tatu. Wa kwanza aliendelea kusumbua na vurugu ziliongezeka nyumbani, maelewano yakatoweka. Mume wangu aliungana na familia yake na kusema mimi ni chanzo na hawakuamini kwamba ni sikoseli. Walidai ni 'chango' (ugonjwa unaowapata watoto unaofanana na degedege).

"Baadaye mtoto wa kwanza akapatwa na degedege. Nilikwenda naye Bugando, nilikaa naye kwa muda wa siku saba, wakamfanyia vipimo ikaonekana figo imeharibika sana kutokana na matumizi holela ya zile dawa za kienyeji. Ikawa ndiyo safari yake ya mwisho duniani... alipoteza maisha.

"Wakati huyo mwanangu akiwa mahututi hospitalini, yule wa pili aliomba kwenda hospitalini kumwona ndugu yake, kipindi hicho naye alikuwa anatibiwa nyumbani kwa miti shamba, wakamkatalia. Alilia hadi akapoteza fahamu. Akalazwa katika kituo cha afya kilichoko maeneo hayo, lakini alipozidiwa tukalazimika naye kumpeleka Bugando.

"Hapo nikawa na watu wawili; mmoja mochwari mwingine chumba cha wagonjwa mahututi, kwa wakati mmoja. Nilikwenda kuzika na baadaye nikarudi kumwuguza huyu mwingine. Hapo familia hatuelewani kabisa.

"Niliamua kuomba uhamisho ili niwe karibu na hospitali hii kwa ajili ya matibabu ya mtoto ambaye alikata kauli tangu kipindi kile akihitaji kumwona ndugu yake, ilimchukua miezi mitatu akiwa anakula kwa mpira. Miezi mitatu baada ya mwenzake kufariki (dunia) naye akaaga dunia... (simanzi inamtawala, anahamia kwenye kilio)."

Baada ya takriban dakika tano, mama huyo anaendelea na mazungumzo na mwandishi, akisimulia: "Baadaye nikajifungua mtoto wa nne. Daktari (wa Bugando) alinishauri niwapime watoto waliobaki hai. Majibu yalipotoka, mtoto wa tatu alionekana kuwa na sikoseli na wa mwisho alikuwa mzima kabisa.

"Daktari alishauri waanze kumshughulikia huyu mtoto wa tatu. Kipindi hicho nilikuwa ninalea mwenyewe. Tulitengana na baba yao kutokana na kunituhumu kwamba mimi ni chanzo kwa vyote vilivyotokea. Alitoa kauli kali kwamba 'heri watoto hao wamefariki dunia maana wamemgharimu kiuchumi," anadai Mwalimu Aman.

Mama huyo anasema anazingatia kliniki ya mwanawe huyo, akibainisha kuwa hakuwahi kufanya uchunguzi wa afya yake. Baada ya kupata matatizo hayo, alipima na majibu yalibainisha ana hali anayoiita "AS", ikiwa na tafsri ya kitabibu kwamba hana selimundu, lakini amebeba chembechembe za maradhi hayo.

Mwalimu Aman anashauri watu wanaoingia katika uhusiano wapime kwanza hali ya vinasaba vyao na kutokupendana kwa macho tu kwa kuwa athari itakayomkuta mtoto watakayemzaa ni kubwa na wakikaidi wakubaliane na matatizo watakayokutana nayo.

"Ninaomba serikali itoe elimu kwa jamii ili iwe na uelewa kuhusu ugonjwa huu kama magojwa mengine sambamba na kupunguza gharama za matibabu, hasa upandikizaji uloto pamoja na kuwa na wataalamu wa ugonjwa huu hadi ngazi ya vituo vya afya na zahanati," anashauri.

Binti wa mama huyo, Anthonia Bundala (10), anayeugua selimundu, mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Nundu, wilayani Ilemela, anaiambia Nipashe:

"Ninamshukuru sana Mungu, mama yangu, ndugu zangu na marafiki zangu shuleni, wananipenda sana. Ninapenda kusoma na mama ananisaida, nina imani ndoto yangu nitaifikia ya kuwasaidia watu wengine wenye ugonjwa kama wangu nitakapokuwa daktari."

**MASHUJAA WA SELIMUNDU**

Priscilla Chassam, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mashujaa wa Sikoseli Tanzania, anasema kuwa katika kutoa elimu ya ugonjwa huo wilayani Busega mwaka jana, walipimwa watu 365. Nusu yao (182) walikuwa na ugonjwa ya selimundu, wengine wana chembechembe za selimundu na wachache hawana chembechembe wala selimundu.

"Hapo utaona jinsi gani ugonjwa huo ulivyo mkali. Tunaendelea kutafuta fedha kuyafikia maeneo mengine ya vijijini," Priscilla anasema.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Selimundu Wizara ya Afya, Dk. Asteria Mpoto anabainisha kuwa serikali inafanya jitihada kuweka unafuu kwenye huduma za selimundu ikiwa ni pamoja na kuimarisha matibabu ya kibingwa ya upandikizaji uloto.

Anasema kuwa kwa kuanzia, serikali imegharamia matibabu ya kibingwa BMH kwa watoto wenye ugonjwa huo kwa kupandikiza uloto ili kuwapunguzia maumivu wanayoyapata.

Elisha John (12), mmoja wa watoto wanane walipona selimundu baada ya kupandikizwa uloto BMH, anasema: "Nilikuwa ninapata shida ya kuumwa kichwa, damu yangu ilikuwa inapungua mara kwa mara. Shuleni nilikuwa simalizi mwezi, lazima nitalazwa. Wiki nzima sihudhurii vipindi shuleni, tangu nimetibiwa sijasikia maumivu yoyote."

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema zaidi ya watu 200,000 nchi wanaugua ugonjwa wa selimundu.

Alikuwa anajibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Fatma Hassan Toufiq aliyehoji idadi ya watanzania wenye selimundu na ni mikoa mingapi iliyoathiriwa zaidi na ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Afya, Dk. Mollel, mikoa iliyoathiriwa zaidi na selimundu nchini ni Mwanza, Tabora, Kigoma, Mara, Dar es Salaam na Pwani.

"Utafiti unaonesha sehemu zenye maambukizi ya malaria kwa wingi, ndizo ambazo pia zina wagonjwa wengi wa selimundu," anasema Dk. Mollel na kubainisha kuwa Tanzania ina zaidi ya watu 200,000 wenye selimundu.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwaka mpya uje na mambo mapya ukusanyaji kodi

**MAENDELEO** ya nchi hayawezi kupatikana bila kodi zinazokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato.

Ujenzi wa barabara za kisasa, hospitali, shule na huduma nyingine muhimu anazotakiwa kupata mwananchi zinatokana na kodi ambazo serikali inakusanya.

Hata hivyo, matokeo ya kodi hizo ni lazima yaonekane ili wananchi waendelee kuona umuhimu wa kulipa kama inavyoonekana katika nchi nyingine duniani zilizoendelea.

Katika nchi zilizoendelea kodi hizo pia husaidia kuwatunza wazee ambao hawawezi tena kujitegemea na badala yake kulelewa kwenye nyumba za kutunza wazee. Hata kwa wale wanaoweza kujitegemea, serikali zao huwalipa kiwango fulani cha pesa kila mwezi ili waweze kununua mahitaji muhimu na kulipa bili mbalimbali za huduma.

Mara nyingi malalamiko hujitokeza wananchi wanapoona wanakatwa kodi, lakini fedha zinaelekezwa kwenye matumizi mengine ambayo hayawagusi moja kwa moja.

Vyanzo vya makusanyo ya kodi viko vingi na kama kila mwananchi angewajibika kuilipa nchi yetu ingekuwa mbali kimaendeleo.

Kwa nchi ambazo zimepiga hatua katika maendeleo, mengi yametokana na kodi zinazokusanywa na serikali.

Wananchi pia wanaelewa umuhimu wa kulipa kodi kwasababu wanaona faida zake katika kuwahudumia kwenye sekta mbalimbali.

Udanganyifu katika ulipaji kodi unarudisha maendeleo na kuifanya serikali kubeba mzigo mkubwa kutekeleza baadhi ya miradi kwa kutegemea ufadhili au mikopo kutoka kwenye nchi zilizoendelea.

Baadhi ya wafanyabiashara hudiriki kufanya udanganyifu kwenye ulipaji kodi kwa kuandika risiti zisizo za uhalisia na bidhaa walizomuuzia mteja.

Uaminifu kwa pande zote za ulipaji na ukusanyaji ni jambo muhimu sana ili kufikia hatua zilizofikiwa na nchi nyingine duniani zilizoendelea. Wakati mwingine uaminifu unakosekana kutokana na walipakodi kuona fedha zao zinatumika vibaya kinyume na makusudio.

Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akihamasisha wananchi kulipa kodi ili nchi iweze kusonga mbele na kukamilisha miradi ambayo imekwama kwa kukosa fedha.

Amekuwa akisisitiza kuwa ili nchi itekeleze miradi ya maendeleo wananchi hawana budi kulipa kodi zinazowekwa na serikali haijalishi ni ndogo au kubwa ili mradi iwe halali.

Tozo ndogo ndogo pia husaidia kwenye mapato na kujenga barabara, madaraja, shule na mambo mengine,

kwa sababu hakuna serikali inayoendeshwa kwa pesa nyingine zozote isipokuwa pesa za kodi za wananchi wake.

Hata hivyo, miradi hiyo pia itunzwe ili iweze kudumu na kunufaisha vizazi vijavyo. Lakini, kuna baadhi ya wananchi hudiriki kuharibu miradi hiyo kwa makusudi na kusababisha hasara ya kuitengeneza tena badala ya kujenga miradi mingine.

Kuna ambao wana tabia ya kuchimba na kulima pembezoni mwa barabara na kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuharibu miundombinu hiyo.


Kilometa moja tu ya barabara ni sawa na kujenga vituo vitatu vya afya vya kata pamoja na kuweka vifaa tiba ndani.

Kuna baadhi ya wanaohujumu miradi hiyo kwa kung'oa vyuma vya kingo vilivyowekwa kwenye madaraja na kwenda kutengeneza vifaa mbalimbali. Ukiangalia gharama iliyotumika kutengeneza kingo hizo na vifaa vinavyotengenezwa ni hasara kubwa. Wananchi hawafahamu sio serikali pekee inayoathirika bali hata wewe ambaye unalipa kodi.

Mara ngapi wananchi wanalalamika tozo zinazokatwa kwenye miamala ya simu, kama miundombinu itaendelea kuharibiwa hakuna shaka kuwa unafuu wa tozo hautakuwapo.

Ni muhimu kila mwananchi kuona uchungu na kuwa mlinzi wa mwenzake ili miradi inayojengwa iendelee kudumu na mingine ijengwe kwa lengo la kuleta maendeleo makubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# 2025 sekondari ziwe na wataalamu wa maabara

**MWAKA** 2024 unafikia tamati leo ili kuupisha 2025 utakaoanza baadaye saa 6:00 usiku. Kabla ya kuingia mwaka mpya, nimeona nigusie jambo moja katika elimu ninalotamani lifanyiwe kazi mwakani.

Kwa miaka nenda rudi, elimu imeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uhaba wa walimu, madarasa, madawati na maabara ambazo ni wazi zinakwamisha maendeleo ya elimu kwa wanafunzi.

Tunapokaribia kuingia mwaka mpya ingawa kuufikia ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu, ninataka kujadili zaidi suala la ukosefu wa wataalamu wa maabara za fizikia, kemia na baiolojia katika sekondari za umma.

Kwanza ikumbukwe kuwa mafanikio katika sayansi huwa yanaanzia kwenye maabara, kwa maana ya wanafunzi kujifunza kwa vitendo kupitia wataalamu wa maabara hizo katika shule wanazosoma.

Lakini pamoja na jitihada za serikali za kuhamasisha ujenzi wa majengo kwa ajili ya vifaa vya maabara, kumekuwapo na changamoto ya ukosefu wa wataalamu wa maabara hizo katika baadhi ya sekondari.

Imekuwa ikielezwa kuwa ukosefu huo husababisha baadhi ya walimu wa masomo ya sayansi kugeuka kuwa wataalamu wa maabara hizo ingawa inawezekana wasiwe na uwezo wa kufundisha kama wataalamu wenyewe.

Kwa kuwa changamoto hii imeendelea kujitokeza, ninadhani ingekuwa ni vyema kama ingeishia mwaka 2024, ili mwaka ujao uwe kuhakikisha kila sekondari ya umma inakuwa na wataalamu hao.

Kimsingi, masomo ya sayansi hayafundishwi kwa nadharia pekee, bali kwa vitendo, hivyo suala la kila sekondari kuwa na wataalamu hao lingepewa uzito badala ya kutwisha mzigo walimu wa masomo hayo.

Miaka ya nyuma kulikuwa na upungufu wa maabara za sayansi katika shule za sekondari za umma, lakini jitihada zikafanyika na zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha sekondari zote zinakuwa na maabara.

Pamoja na jitihada hizo, kikwazo kilichoko ni ukosefu wa wataalamu hao, hali ambayo huenda ikasababisha nchi kukosa wataalamu bora wa baadaye kutokana na ukosefu wa wataalamu hao.

Iwapo hakuna uwezekano wa kupata wataalamu hao, ninadhani ingekuwa ni vyema walimu ambao hutumia maabara hizo wapewe mafunzo ili wasaidie wanafunzi kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo.

Hilo likifanyika linaweza kupunguza ombwe lililopo la ukosefu wa wataalamu hao katika sekondari za umma ili wanafunzi waweze kusoma masomo ya sayansi kwa vitendo, hasa ikizingatiwa kuwa kwa kawaida mafanikio ya sayansi huwa yanaanzia kwenye maabara.

Walimu wanaotumia maabara hizo, wameonyesha jinsi ambavyo wanaweza kusaidia wanafunzi angalau kwa kiasi cha uelewa walionao, hivyo wakiongezewa ujuzi wanaweza kuwa wazuri zaidi katika matumizi ya maabara hizo ambazo kwa sasa ziko karibu kila sekondari.

Ujuzi wao mdogo walionao wa matumizi ya maabara, wakiongezewa wanaweza kuwa wazuri zaidi katika ufundishaji kwa vitendo na hivyo kuwasaidia zaidi wanafunzi wao.

Walimu wasio na ujuzi wa kutosha wa kutumia maabara, msaada wao kwa wanafunzi unaweza kuwa mdogo, hivyo wangeongezewa ujuzi zaidi ili wasaidie wanafunzi wakati serikali ikiendelea kujipanga.

Wakati kukiwa na changamoto hiyo, nyingine ni hii; kwamba baadhi ya shule zina maabara na wataalamu wake, lakini hazina walimu wa masomo hayo. Hiyo nayo ni changamoto ya miaka nenda miaka rudi.

Ingekuwa ni vyema kama changamoto hizo zingebaki kuwa historia kuanzia mwaka 2025 ili kuwapa fursa wanafunzi kujifunza masomo ya sayansi kikamilifu bila changamoto yoyote inayowakwamisha.

Nchi inahitaji wataalamu wa baadaye waliobobea katika fani mbalimbali, hivyo bila kuwekeza kwa wataalamu wa maabara na walimu wa masomo hayo, itakuwa ni vigumu kuandaa vizuri wataalamu hao wa baadaye.



Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Tumaini Sebastian (wa tatu kushoto), akikabidhi zawadi za mwaka mpya mbuzi wawili, mchele kilo 100, sukari kilo 25, unga wa ngano kilo 25 na lita 20 za mafuta ya kupikia, zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa watoto yatima na wenye uhitaji maalum wa kituo cha Light In Africa cha Mji mdogo wa Mirerani jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vituo 47 vyaanzishwa kufundisha Kiswahili

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI kupitia Baraza la Kiswahili Tanzania imeanzisha vituo 47 vya kufundisha lugha ya Kiswahili ili kukuza na kueneza lugha hiyo duniani.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Profesa Paramagamba Kabudi, alisema hayo wakati akifungua Kongamano la kimataifa la utamaduni lijulikanalo Afrika ya kesho Cultural International lililofanyia katika Chuo Kikuu cha Jordan (JUCO), mjini Morogoro.

Alisema kati ya vituo hivyo vya kufundishia lugha ya Kiswahili 17 viko nje ya Tanzania na 30 hapa nchini.

Profesa Kabudi alisema kuwa Taasisi za elimu ya juu kupitia vijana wanaendelea kufanya utafiti na kuibua mijadala ya kutafuta urithi wa utamaduni unaoshikika na usioshikika.

Alisema kuwa lengo ni kusaidia kurudisha uthamani wa kiafrika kwa maslahi mapana ya Bara la Afrika.

Naye Msemaji Mkuu wa Kongamano hilo linaloandaliwa na vyuo vikuu na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya Tanzania, Profesa Anna Tibaijuka, alisema kuwa na lugha moja ya asili inabeba vitu vingi vya kiutamaduni na haitakiwi kukipoteza Kiswahili kwa kufuata lugha za kigeni.

"Lazima tulinde Kiswahili, lakini na lugha zetu za makabila yote, na kwenye hili lazima tusiweke ukabila," alisema Profesa Tibaijuka.

Mkuu wa Chuo kikuu cha Jordan, Profesa Bertram Mapunda, alisema kuwa kizazi cha sasa kinaamini kuwa mambo ya utamaduni na kuzungumza lugha za asili ni ya wazee wa zamani, aliwasihi na kuwataka vijana kujifunza lugha za asili ili kusaidia kukuza na kueneza lugha hiyo.

Profesa Mapunda alisema chuo kikuu hicho kinakusudia kuanzisha mitaala watayoweza kuingiza kufundisha lugha za asili kwa wanafunzi ili kuendelea kukuza na kueneza lugha hizo.

Naye kiongozi wa kimila kutoka kabila la Maasai, Chifu Mtayani Simanga, alisema kupitia kongomano hilo viongozi wa asili walikusudia kuonana na viongizi wa nchi ili kuwaeleza namna sahihi ya watu wanavyotakiwa kuishi majumbani ili kurejesha hali ya amani na utulivu katika bara la Afrika.

Mdau Adam Ole Mwarabu, alishauri serikali kuzielekeza shule kufundisha lugha za asili ikiwamo Kiswahili ili kusaidia kuondoa lugha za kigeni zilizoletwa na wakoloni.

"Iwapo tutatumia lugha hizi za asili katika maeneo yetu mbalimbali itasaidia kujenga na kuongeza upendo, umoja, mshikamano na amani katika nchi yetu hasa kwa watu wanaofanya ubaguzi wa makabila," alisema Ole Mwarabu.

Kongamano hilo limeandaliawa na Chuo Kikuu cha Jordan kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM), Chuo Kikuu cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Zimbabwe, Chuo kikuu cha Nigeria naTaasisi ya Arizona ya Marekani (PPEP).

Mambo Mbalimbali yalijadiliwa katika kongamano hilo ikiwamo yanayohusu masuala ya lugha, siasa, uchumi, utamaduni, maadili, historia, urithi, haki na mada kubwa ni jitihada za jamii kuhusu uhifadhi wa utamaduni wa kiafrika.

# PM aridhishwa mafanikio Wilaya ya Ruangwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema kuwa Wilaya ya Ruangwa imepiga kasi kubwa ya maendeleo ambayo imewawezesha wakazi wa wilaya hiyo kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Alisema kuwa wilaya hiyo changa ilikuwa na changamoto nyingi kwenye Sekta ya Elimu, Afya, Kilimo, Miundombinu ikiwamo barabara, maji, umeme, uwekezaji na hata kwenye michezo "Changamoto hizi zilitufanya tuje na kaulimbiu ya "Ruangwa kwa Maendeleo Inawezekana, na sasa imewezekana."

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati alipozungumza na mamia ya wakazi wa kijiji ya Mbekenyera, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Alisema kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya wilaya hiyo kutokana na fedha ambazo amekuwa akitoa zilizowezesha kutekeleza miradi hiyo ya kimkakati.

Akizungumza kuhusu Sekta ya Elimu, Majaliwa alisema Wilaya ya Ruangwa ilikuwa na vijiji vichache kati ya tisini vilivyokuwa na shule za msingi, lakini hivi sasa kila kijiji kina shule ya msingi "Na tunaendelea kujenga kwenye vitongoji".

"Kwa upande wa shule za sekondari tumemaliza kata zote kujenga shule za sekondari kwenye wilaya hii na tunachokifanya sasa ni kuongeza shule kwenye kata zenye msongamano mkubwa na hapa Mbekenyera tulikuwa na shule ya Tarafa, lakini baada ya kuona kuna msongamano wa wanafunzi, tumejenga shule nyingine pale Mkutingombe".

Aidha, alisema kuwa Sekta ya Afya katika wilaya hiyo imeimarika kwa kiasi kikubwa kutokana na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya pamoja na ujenzi wa hospitali ya wilaya ambayo ina uwezo wa kutoa hadi huduma za kibingwa

Kadhalika, wilaya hiyo imefanikiwa kujenga mtandao wa barabara za lami katika maeneo mbalimbali na mpango wa kuendelea kujenga barabara za lami unaendelea "Itakuja barabara ya kutoka Masasi kwenda Kiranjeranje, na sasa Masasi kwenda Nachingwea mkandarasi yupo, Ruangwa kwenda Nachingwea, mkandarasi yupo na ameanza kazi na tunajenga kilomita 21 kutoka Ruangwa mjini mpaka Namichiga kwa kiwango cha lami".

Alizungumzia sekta za, kilimo, maji na uwekezaji na kusema kuwa kazi kubwa imefanyika na serikali inaendelea kuziwekea mikakati endelevu sekta hizo "Kwenye sekta ya nishati, tumeshapeleka umeme kwenye vijiji vyote na sasa tunaenda kwenye mradi wa vitongoji, ndugu zangu wananchi, tumeshapeleka laini, ni wakati wenu sasa kuvuta umeme".

Awali, alitembelea kiwanda cha kubangua korosho cha Naunambe Cashewnuts kinachomilikiwa na mwekezaji mzawa Juma Chambone na kina thamani ya Sh. milioni 250. Kiwanda hicho kipo katika kijiji cha Mbekenyera.

Pia, aligawa vifaa vya muziki vyenye thamani ya Sh. milioni 20 kwa bendi ya Mkurupuko Jazz iliyopo kwenye kijiji cha Mbekenyera.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wamtakia Rais Samia heri kwa uongozi wenye uadilifu

**Na Steven William,**
MUHEZA

KUELEKEA Sikukuu ya Mwaka Mpya 2025, viongozi wa umma na Watanzania wamemtakia heri Rais Dk. Samia Suluhu ambaye ameonesha utendaji kazi mzuri, uadilifu kwa maslahi ya taifa.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini na mbunge mstaafu wa Jimbo la Muheza, balozi Adadi Rajabu, alisema Rais Samia amefanya kazi kubwa ya kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali na kudumisha amani nchini.

Balozi Adadi alisema kwa kipindi cha muda mfupi ameonesha njia ya ushirikiano mzuri Tanzania katika sekta mbalimbali pamoja na kuwakaribisha wawekezaji nchini kufungua uchumi.

Alisema kuwa Watanzania wenyewe wameona utendaji kazi wa Rais kujenga barabara, shule, sekta ya afya hospitali, kuboresha sekta ya maji, umeme, barabara na reli ya SGR.

Mchungaji kiongozi wa kanisa la KKKT Usharika wa Muheza Tanga, Elias Majo, alisema wanamshukuru Mungu kwa kujalia uzima mwisho mwaka huu ni wa kujitathimini kuanzia kaya, wilaya, mkoa hadi taifa kuendelea kumshukuru Mungu.

Padri wa kanisa la Romani Katoliki la Kristo Mfufuka wilayani Muheza, Martine Kihiyo akizungumzia suala la kulinda amani alihimiza Watanzania kuheshimu, kulinda amani na utulivu katika nchi badala ya kutumika kuharibu tunu hiyo muhimu akisistiza kusameheana kutokana na upungufu wa kibinadamu na kuanza mwaka upya kwa upendo na mshikamano.

"Sisi hatuna cha kumlipa Mungu zaidi ya kufanya toba, majuto na kujiongeza zaidi kumjua Mungu na uwe mwaka wa kudumisha amani sio kupanga kuvuruga kama tumeishi vyema mwaka uliopita tujiulize tulitumia vigezo gani kuwa salama hadi sasa?" Alieleza Mchungaji.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana mtaa wa Madaba, wilayani Muheza alisema ipo sababu ya kila mmoja kumshukuru Mungu kwa kulipigania taifa mwaka 2025 kusheherekea kwa amani.

"Nitoe salamu za kheri ya mwaka mpya na tunapoanza waumini wa imani zote tufanye kazi kwa bidii kuunga juhudi za serikali kuinua uchumi wetu, wazazi na walezi nao niwasihi kuwalea watoto wao katika maadili mema kwani ndiyo nguvu kazi ya taifa kwa siku zijazo," alifafanua mchungaji Luhinga.

Mkuu wa Jeshi la Polisi Usalama barabarani Wilaya ya Muheza, Leonard Bandola alitoa onyo kwa baadhi ya watu watakaofanya fujo au vitendo vya uhalifu wakati wote hasa kipindi cha sikukuu akisema jeshi halitomfumbia macho mtu huyo.

"Sisi Jeshi tuko imara kuhakikisha watu wanasherehekea salama na tumeshirikisha wenye nyumba za wageni, vikundi vya ulinzi shirikishi kutoa taarifa za watu ambao wanawatilia shaka, tuna doria za magari, miguu na tuwatake wazazi kuwa makini na watoto wao," alisisitiza Bandola.

Juma Athumani mkazi wa Muheza aliishauri jamii kupendana na kushirikiana katika shughuli za uzalishaji kwa kupeana fursa za kiuchumi kujiletea maendeleo kwa mwaka ujao.



Gari likiwa limepinduka na kuziba njia kutokana na ubovu wa barabara ya kuelekea Goba Tegeta A, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# BoT yasisitiza matumizi kidijitali malipo kibenki

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imewashauri watumiaji wa huduma za kibenki, kuendelea kutumia malipo kwa njia ya kidijitali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Gavana ya BoT, Emmanuel Tutuba, benki hiyo itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhamasisha matumizi ya malipo ya kidijitali nchini.

Alisema katika kufanikisha hilo, itahakikisha kuwa malipo yanayofanywa kwa kutumia mashine za malipo za wafanyabiashara (POS), yanafanyika bila malipo kwa watumiaji wa kadi.

"Mojawapo ya hatua hizo ni kuhakikisha kuwa malipo yanayofanywa kwa kutumia mashine za malipo za wafanyabiashara (Point of Sale -POS) ni bure kabisa kwa watumiaji wa kadi," alisema Tutuba katika taarifa yake kwa umma.

"Benki Kuu ya Tanzania, inapenda kuwakumbusha wananchi kwamba malipo yanayofanywa kwa kutumia kadi za benki (debit, credit, au prepaid) kwenye mashine yeyote ya POS hayatozwi ada yoyote. Wafanyabiashara wote wamekatazwa kutoza ada au gharama za ziada kwa miamala inayofanywa kwa mashine za POS."

Alisema Benki hiyo inawahimiza Watanzania kuendelea kutumia mifumo ya malipo ya kidijitali, kwa kuwa ni njia salama, rahisi na yenye gharama nafuu ya kukamilisha miamala.

"Matumizi ya mifumo ya kidijitali, ikiwamo kadi za malipo, huchangia kujenga uchumi wenye matumizi kidogo ya pesa taslimu, na pia huleta faida kama usalama, uwazi na urahisi wa matumizi," alisema Tutuba.

"Iwapo mlipaji utatakiwa kulipa ada au gharama za ziada unapotumia mashine yoyote ya POS, tafadhali toa taarifa kwa benki yako au wasiliana na Dawati la Malalamiko la Wateja wa Benki Kuu ya Tanzania."

# Nyumba za w'kazi wa afya kukamilika Jan. 2025

**Na Sabato Kasika**

MRADI wa ujenzi wa nyumba za makazi ya wafanyakazi wa afya karibu na Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini B, eneo la Pangatupu, Mkoa wa Kaskazini Zanzibar unatarajiwa kukamilika Januari mwaka 2025.

Ujenzi huo unaogharimu Shilingi bilioni nne, ulianza Januari, mwaka huu, unahusisha jengo moja la ghorofa tatu litakalohudumia na familia 16 ukijumuisha familia nane za vyumba vitatu vitatu na familia nane za vyumba viwili viwili vinavyojitegemea kwa kila familia.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Matibabu Dk. Mngereza Miraji, alisema hayo katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi nyumba za wafanyakazi hao mbele ya mgeni rasmi Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi, Riziki Pembe Juma.

"Ujenzi wa makazi hayo ni kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ukikamilika unatarajiwa kugharimu takribani Shilingi bilioni nne za Kitanzania na ulianza Januari 2024 na unatarajiwa kumakamilika Januari 2025," alisema Dk. Miraji.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Riziki alisema Serikali ya awamu ya nane inaendelea kuimarisha huduma za afya ili kuhakikisha wanannchi wanapata huduma za afya bila usumbufu.

Alifafanu kuwa katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2020/2025, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuchukua hatua kadhaa za kuimarisha huduma za afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo mapya ikiwamo nyumba za wafanyakazi na kuweka vifaa vya kisasa.

"Wakati kampeni za uchaguzi wa mwaka 2020, CCM iliahidi na sasa serikali inatekeleza ahadi kwa vitendo kwa ajili ya kutoa huduma bora za afya kwa wananchi na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya dharura ili kupunguza vifo visivyotarajiwa," alisema.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kusimamia na kuhakikisha watoa huduma wa afya wanapatiwa makazi mazuri ili kutoa huduma bora kwa wananchi."

Alisema hatua ya serikali kujenga makazi ya wafanyakazi karibu na hospitali inawapunguzia wafanyakazi masafa na kupunguza gharama za ufasiri za kufuata madaktari bingwa katika makazi yao.

"Nyumba hizo zinatarajiwa kuchukuwa familia 16, uongozi wa Wizara ya Afya ingeanza kufikiria utaratibu mzuri utakaoutumika kuzitunza ziweze kutumika vizuri ikiwamo kuzifanyia ukarabati kwa wakati," alisema.

Mkuu wa Wilaya Kaskazini B, Juma Sururu Juma, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja alimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuwajengea majengo hayo na miradi mengine inayotekelezwa katika mkoa huo.

## BAKWATA wahamasisha matumizi GPS

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SHEHE wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), mkoani Kilimanjaro, Shaaban Mlewa, amesema serikali inapaswa kuharakisha mchakato wa matumizi ya kifaa maalumu cha kukokotoa mawasiliano ya kijiografia (GPS).

Amesema lengo ni kuzisukuma halmashauri za wilaya kukitumia kuilinda miti yote inayopandwa na wadau wa uhifadhi wa mazingira.

BAKWATA Kilimanjaro, imejitosa kupanda miti 5,000 na kuingia moja kwa moja katika orodha ya wadau wanaohifadhi mazingira na urejeshaji wa baionoai katika maeneo yaliyoharibiwa na shughuli za binadamu.

Mlewa aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mpango mkakati wa BAKWATA wa upandaji miti kimkoa, uliofanyika katika Zahanati ya Bomang'ombe, Wilaya ya Hai. Mpango huo unakwenda sambamba na maadhimisho ya Sikukuu ya Maulid.

Baada ya kuzindua mpango huo, Mlewa, aliagiza mashehe wa wilaya zote mkoani humo kusimamia na kuhakikisha miti iliyopandwa inakua na kuachana na kasumba iliyozoeleka ya kupanda miti na kuitelekeza.

"La kwanza, GPS ambayo wadau wa mazingira wamekuwa wakitaka itumike, ni kweli ina uwezo wa kulinda uharibifu wa miti yote inayopandwa kwa kurekodi matukio yote yanayoendelea na kupeleka kwenye mfumo wa satelaiti na teknolojia ya GPS. Hivyo, ni vizuri mamlaka husika ikaharakisha matumizi yake.

"Jambo la pili, mashehe na taasisi nyingine zinazopanda miti, tuzingatie maelekezo na kusimamia miti yatakayopanda inakua na kufikia malengo yaliyokusudiwa ya Tanzania ya kijani."

Kwa mujibu wa Mlewa, amelazika kusema hivyo, kwa kuwa kuna kasumba iliyozoeleka ya watu kupanda miti bila kugeuka nyuma kuangalia kama miti hiyo imekua, jambo ambalo sio zuri.

Alisema iko kasumba, viongozi na baadhi ya wananchi wakishapanda miti na kupiga picha ili kuonekana wameipanda, huondoka na hawarudi kuihudumia tena, hatimaye miti hiyo hufa.

# Wa-Rombo 'wafundwa' kuchangamkia fursa

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

MTAALAMU wa masuala ya uchumi na uwekezaji nchini, Dk. Genuine Shirima, amewapa 'shule' wazawa wa Rombo wanaoishi ndani na nje ya Tanzania kuyaishi maono yao kwa kuchangamkia fursa za uwekezaji.

Amewataka kuchangamkia fursa za uwekezaji katika dhamana za serikali, hati fungani za kampuni, hati fungani za miundombinu ya barabara za wilaya maarufu 'Samia Infrastructure Bond'.

Dk. Shirika, alitoa darasa hilo la uwekezaji juzi katika eneo la Mashati, Kata ya Katangara Mrere, Rombo, mkoani Kilimanjaro, wakati wa mkutano mkuu wa kwanza wa Rombo Unity (RU), uliowakutanisha wanachama 410.

Kuna maeneo mengi ya kuwekeza kama dhamana za serikali, hati fungani za kampuni, hati fungani za miundombinu.

"Niwadokeze tu kwamba hizi hatifungani dirisha limeshanguliwa tangu Novemba 29 mwaka huu na linakwenda hadi Januari 17 mwaka 2025. Kianzio ni Shilingi 500,000 na kuendelea, wakati riba ni asilimia 12 kwa mwaka.

Gawio lake ni mara nne kwa mwaka, hakuna makato ya kodi na uwekezaji wake hudumu kwa kipindi cha miaka mitano. Tufikirie zaidi kuwekeza kwenye uwekezaji katika ujenzi nyumba na mashamba makubwa, ambao uwekezaji wake una faida ya asilimia 16.

Hadi kufikia Desemba 27 mwaka huu, Rombo Unity iliyoanzishwa miezi 20 iliyopita, licha ya kugharamia shughuli 44 za mazishi, ilikuwa imewekeza Sh. milioni 70 kwenye UTT AMIS (Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali Tanzania).

Katibu Mkuu wa Rombo Unity, Anthony Kawishe, alisema umoja huo ulianzishwa Mei mwaka 2023 kutokana na wana Rombo wengi kuwa kwenye mahangaiko ya kukabiliana na changamoto zao kadhaa, hasa za msiba pindi inapojitokeza.

Kwa mujibu wa Kawishe, Rombo Unity, imejengwa kwa mfumo wa kitaasisi na siyo kama mali ya wachache kutokana na namna inavyofanya kazi na kujiendesha kwake.

Alisema: "Malengo yetu ni kufanya mageuzi makubwa ya kijamii na kiuchumi na kufikia lengo la kuwa taasisi kubwa ya kuigwa ndani na nje ya Rombo katika nyanja za kiuchumi na kijamii".



Dereva wa bodaboda wilayani Muheza mkoani Tanga, Athumani Waziri, akitoa mipira ya kiume (kondom) kwa ajili ya kutoa elimu kwa wenzake kuhusu umuhimu wa kutumia ili kuepuka maambukizi ya virusi vya Ukimwi jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wakulima waeleza utamu wa mradi wa AID-I

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MRADI wa kupeleka teknolojia haraka kwa wakulima (AID-I), unaotekelezwa na Shirika la Floresta Tanzania, kwa kushirikiana na World Vegetable Center, umeanza kuonyesha matunda, baada ya wakulima kueleza namna wanavyoridhishwa na upatikanaji wa mbegu na miche bora ya mboga.

Licha ya kurahisisha upatikanaji wa mbegu, pia umewasaidia wakulima kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya mboga, matunda, viungo na kuboresha lishe ya jamii.

Wakizungumza jana katika Kijiji cha Embukoi, Kata ya Donyomoruwa, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Lekishon Mollel, ambaye ni mwenyekiti wa viongozi wa mila wa wafugaji wa jamii ya Kimasai (Leigwanani), alisema kutatuliwa kwa changamoto hiyo kunaongeza tija na ufanisi wa kuwa vyanzo vya uhakika vya usalama wa chakula.

"Kwa mfano leo ukiangalia maeneo yote ya ukanda huu, hakuna malalamiko ya wakulima kukosa mbegu na miche bora ya mboga. Kupitia mradi huu, sasa wamasai wanakula mlo kamili, unaojumuisha mboga na matunda na hivyo kupambana na changamoto za lishe duni miongoni mwa jamii, hasa kwa vijana balehe," alisema Mollel.

Mwenyekiti wa kikundi cha wakulima cha kuweka na kukopa cha Emusoi, Jackson Laizer, alisema wanayaona mabadiliko makubwa katika lishe kwenye jamii yao, kwa kuwa Shirika la Floresta Tanzania, limewaelimisha wafugaji wa kimasai kula mboga.

Mradi huo wa AID-I), unafadhiliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID).

Mkurugenzi wa Shirika la Floresta Tanzania, Richard Mhina, alisema mradi huo wa AID-I, unalenga kuwafikia watu 5000 kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo asilimia 60 ni


vijana na asilimia 40 ni watu wazima.

Aidha, alisema mradi huo sio tu unalenga kuongeza uwezo wa kiuchumi wa makundi hayo, bali pia kuwezesha vijana na wanawake kuwa wahamasishaji wakuu wa sekta ya kilimo na maendeleo ya kijamii.

Mradi wa AID-I, ni sehemu ya mpango wa kimataifa chini ya msaada wa Serikali ya Marekani (USAID) wa kukabiliana na njaa na umasikini, ukilenga zaidi kutoa msaada kwa wakulima wadogo katika nchi za Tanzania, Malawi na Zambia, kuhakikisha wanapata teknolojia, ubunifu na taarifa zinazohitajika haraka ili kuongeza na kuimarisha uzalishaji wa chakula.

Aidha, Mhina, alisema mradi huo wa AID-I, unalenga kuwafikia watu 5,000 kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo asilimia 60 ni vijana na asilimia 40 ni watu wazima.

Aidha, alisema mradi huo siyo tu unalenga kuongeza uwezo wa kiuchumi wa makundi hayo, bali pia kuwezesha vijana na wanawake kuwa wahamasishaji wakuu wa sekta ya kilimo na maendeleo ya kijamii.





# Samia atoa msaada kwa yatima, wenye uhitaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewakumbuka watoto yatima na watu wenye uhitaji katika Halmashauri ya Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, kwa kuwapatia mahitaji mbalimbali ili waweze kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Paul Chacha alikabidhi msaada huo kwa niaba ya Rais Samia katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Mvuma kilichopo Kata ya Nyasubu.

Chacha alisema Rais Samia amekuwa na utaratibu wa kuwapatia mahitaji mbalimbali watoto yatima wanaoishi katika mazingira magumu, wajane na watu wenye ulemavu kila mwaka.

Chacha ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora alisema Rais Samia amekuwa akifanya hivyo ikiwa ni sehemu ya kuwapatia faraja ili na wao washerehekee sikukuu za mwisho wa mwaka kama yalivyo makundi mengine.

Alitaja mahitaji yaliyokabidhiwa kwa makundi hayo ni pamoja na mafuta ya kupikia, sukari, mchele na mahitaji ya shule kwa watoto wanasoma shule za msingi na sekondari.

Baadhi ya vitu hivyo ni madaftari na kalamu na kuwataka wenye uwezo kuyafikia makundi na kuyasaidia mahitaji muhimu.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Masoud Kibetu aliwasihi wananchi na jamii kwa ujumla kuendelea na utaratibu kuwajali watoto hao wenye mahitaji kwani wengi wameshindwa kutimiza ndoto zao za kielimu kwa kukosa mahitaji.

Msimamizi wa Kituo Mvuma, Laurine Noel alisema, mahitaji yaliyotolewa na Rais Samia yatawasaidia kupunguza changamoto za ukosefu wa chakula kituoni.

Alisema pia kwa wanafunzi waliokuwa wanahitaji mahitaji ya shule watapata ili wakasome na kutimiza ndoto zao kwani wamekuwa wakifanya vema kwenye masomo yao.

Laurine alisema watoto hao wamekuwa wakihitaji mahitaji mengi ila kikubwa zaidi ni chakula na kuwaomba watu wenye uwezo kujitokeza na kuwasaidia ili waondokane na kuomba mara kadhaa.

Alisema asilimia kubwa ya watoto wanaowalea ni wale wanaotelekezwa na ndugu wakiwa bado ni vichanga, hivyo mahitaji ni makubwa.

"Tunampongeza Rais Samia kwa kuwakumbuka na kuwapatia mahitaji muhimu, kituo hiki kina watoto 40 kati yake wasichana 27 na wavulana 14 na wanafunzi wanahitaji mahitaji ili wasome na kutimiza ndoto zao," alisema.





Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Mboni Mhita (wa pili kulia) ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, akikabidhi kitoweo cha mbuzi na vyakula mbalimbali kwa watu wenye uhitaji wilayani Kishapu juzi, ambavyo vimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya sikukuu ya Mwaka Mpya. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vijiji 14 kunufaika mpango matumizi bora ya ardhi

**Na Alphonce Kabilondo,** NYANG'HWALE

VIJIJI 14 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale mkoani Geita vinatarajiwa kunufaika na mipango ya matumizi bora ya ardhi na kuondokana na migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

Mpango huo ulitambulishwa juzi na Ofisa Mipango Miji na Vijiji Mwandamizi, Samora Makoi kutoka Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC) katika Kata ya Nyang'hwale.

Makoi alisema kuwa tume hiyo kwa kushirikiana na halmashauri hiyo inatarajia kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 14 vilivyopo katika Kata ya Nyabulanda, Shabaka na Nyang'hwale.

Alisema kuwa mpango huo utahusisha utengaji wa maeneo ya shughuli mbalimbali za wananchi ikiwemo kilimo, malisho ya mifugo makazi pamoja na maeneo ya huduma za jamii na mahitaji mengineyo kutokana na uhitaji wa wananchi.

Makoi alisema lengo la uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji hivyo ni kuwawezeshwa wananchi kuepuka miingiliano ya matumizi ya ardhi ambayo imekuwa chanzo cha kuibuka kwa migogoro ya mara kwa mara na kuchangia shughuli za maendeleo kusuasua.

Alisema uandaaji wa mpango huo unatarajiwa kuwawezesha wananchi hao kutumia ardhi zao kwa tija ili kuongeza uzalishaji katika shughuli mbalimbali kutokana na elimu watakayoipata kabla ya zoezi hilo kuanza.

Alisema baada ya mpago huo kukamiliika maeneo ya vijiji hivyo yatapimwa na wananchi kupatiwa hati miliki za kimila.

Ofisa Ardhi mwandamizi, Mkwaya Nsongo kutoka tume hiyo akitoa elimu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa wananchi wa kijiji hicho alisema wameamua kuwashirikisha wananchi katika uandaaji wa mpango huo ili waweze kuchangamkia fursa na kuondokana na migogoro ya ardhi.

Diwani wa Kata ya Nyang,hwale, Agatha Malugumba aliwaonya viongozi wa serikali ya kijijiji kutokwenda kuibua migogoro na badala yake wakafanye kazi zao kwa weledi bila kuonea watu au mtu.

## Msharika ajiapisha kuwa askofu, mgogoro wafukuta

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

KATIKA hali isiyo ya kawaida msharika mmoja katika Kanisa la African Israel Nineveh (AINC), Isaya Yusto amejiapisha kuwa askofu wa kanisa hilo kinyume na utaratibu wa kanisa wa kupata nafasi hiyo.

Hali hiyo imezua mgogoro kati ya viongozi wa kanisa hilo na baadhi ya waumini.

Akizungumzia sakata hilo, Askofu Mkuu wa Kanisa hilo lenye makao makuu Kisumu nchini Kenya, John Mweresa alisema muumini huyo alichukua uamuzi huo akishirikiana na baadhi ya viongozi ambao waliendesha makabidhiano ya madaraka kinyume cha Katiba.

Alisema kwa sasa uongozi huo ni batili na hawaruhusiwi kutekeleza majukumu yoyote ya dhehebu hilo kwa kuwa wanadaiwa kughushi nyaraka na baadhi ya vitendea kazi ikiwemo mihuri na nembo.

Juhudi za makundi hayo mawili kutafuta suluhu katika Kituo Kikuu cha Polisi Sirari mwishoni mwa wiki hazikufanikiwa baada ya kuelezwa na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Sirari (OCD) Chausiku Masasi kwamba hakuna viashiria vya jinai.

Akieleza chanzo cha mgogoro huo, Askofu Mweresa alisema miezi miwili iliyopita kanisa lilifanya uteuzi halali wa askofu mwandalizi aitwaye Franco Stingo lakini zoezi la kumuapisha lilivurugwa na kundi la upande wa pili.

Alitahadharisha kwamba watachukua hatua za kimahakama kutafuta nafuu ya kisheria kudhibitisha kuwa ukiukwaji wa Katiba ya Kanisa umefanyika na kuzuia uongozi uliopatikana kwa kujiapisha kinyume na utaratibu.


Yusto anayedaiwa kujiapisha aliiambia Nipashe kwamba wamebadilisha Katiba ambapo pamoja na mambo mengine iliteganisha madaraka ya viongozi wa kanisa hilo nchini pamoja na wale wanaotoka Kenya.

Alisema: "Tulibadilisha katiba ambayo iliwezesha kukabidhiwa madaraka ya jimbo kwa askofu kiongozi kutoka Tanzania na kukomesha utaratibu wa kupokea maagizo kutoka nchi jirani kwenye cheo sawa na hicho kinachopatikana hapa hapa nchini".

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 31, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 13



WASOMI WAAMBIWA
Kukariri nadharia pekee hakutoshi wajue udereva, lugha nyingi na uthubutu

Ukurasa 14



Wenye ushawishi mkubwa 2024

NA MWANDISHI WETU

KWA HERI 2024

# Kumbuka mwaka haubadilishi chochote ni wewe unayebadilisha fikra zako, anza

• Jipe maisha bora usiishi kama jana

KWAHERI 2024 karibu mwaka mpya. Mioyo ya watu imejaa shukurani kwa Mungu ambaye amewapa nafasi ya kuishi hadi leo.

Wapo wenye uchungu wa magonjwa, misiba na taabu lakini wote wamshukuru Muumba maana ni mapenzi yake kwao.

Kwa ujumla mwaka haubadilishi kitu kinachobadilika ni fikra au mawazo yako. Nyakati na majira zinabakia zilivyo. Usiku na mchana vitaendelea kuwepo, pia jua, mbalamwezi , joto mvua ni vya kudumu.

Ila wewe unabadilika kujipa maisha bora zaidi na kuongeza bidii ili usiishi kama ulivyokuwa mwaka jana. Kumbuka ni fikra zako ndizo ziwe mpya siyo mwaka mpya 2025. Kuwa na maono, mawazo na mitizamo chanya na mipya zaidi.

Unapoanza mwaka usitafute lawama mbona sijafanya hiki, sina nyumba, fedha wala mke au mume, mtoto tena wengine wakilalama nina watoto wa kike tu nitapataje wa kiume. Acha maana kuna wasio na watoto.




### JITATHIMINI LEO

Unapoikaribisha 2025 cha muhimu ni kujitafakari na kujitathimini mwenendo wa maisha yako. Inapendeza kama utachukua karatasi na kalamu upitie suala moja hadi jingine na kwa kila hatua ibua ubovu, udhaifu, mafanikio na panga kubadilika.

Unaweza kujihoji hasa kwenye uhusiano na watu wengine kuanzia mwenza, ndugu wa damu, watoto, majirani na wafanyakazi ofisini au wengine unaoishirikiana nao katika kazi zako.

Jiulize swali hili, mimi ni mtu wa msamaha au ni wa kisasi muda wote? Ujijibu ukiona una upungufu jirekebishe mwaka huu. Kuendeleza tabia hiyo kunasababisha shida afya ya akili.

Unyenyekevu, jipime wewe ni mtu mnyoofu au ni jeuri, unashiriki kwenye mambo ya jumuiya, majirani ama unafanya ubabe wakati wote? Unawaudhi wenzake kila mara? Dhamiria kubadilika 2025.

Chunguza udhaifu wako unashiriki kwenye masuala ya kijamii mfano mtaani kwako kuna misiba, majanga kama moto unajihusisha? Kwenye jumuiya watu wa kijijini kwako unashirikiana nao kwenye shida na raha?Unatoa michango ya misiba na kushirikiana na wengine kwenye raha na shida?

Jihoji kuhusu akiba unaweka akiba? Iwe mali au fedha kama huna anza sasa na uwe na nidhamu ya fedha. Wakati mwingine unafurahia kuitwa 'maskini 'Si jambo jema.'

Mfano kama familia inachangisha fedha kujenga mfuko wa kujitegemea, halafu wakakubaliana kila mmoja atoe Shilingi 100, 000 lakini wasio na kipato watoe 20,000 usikubali jitutumue ndiko kuepuka kuitwa maskini. Tafuta pesa kwa juhudi zaidi na kwa njia halali

### ANGALIA FURSA

Tafuta fursa kumbuka kuwa maisha yana fursa na kila mmoja ana nafasi anazopata akazifanyia kazi au akazichezea.Tathmini juhudi zako kwenye kutumia nafasi ulizopata za kuongeza kipato na kubadili maisha.

Chunguza umezitumiaje fursa mwaka jana? Umechezea au umenufaika? Kwa vipi ziainishe kisha uangalie mbele mwaka huu.

Uligeuza changamoto kuwa fursa kujiletea maendeleo? Azimia kuwa mwaka huu changamoto zitakuwa fursa kwa mfano, ukiachwa na mwenza sitakubali kulia, nyanyuka fikiria cha kufanya badala ya kukata tamaa na kuanza matendo ya kumkomoa.

Mfano mzazi aliwakataa watoto wake na kumtelekeza mama yao. Hakuwaendeleza kimaisha hawakusoma wala kuwa na kipato. Hiyo ni changamoto vijana wekeni juhudi fanyeni kazi zaidi ili kuitu-

INAENDELEA UK. 12

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**

# Ndivyo unavyolinda ubongo kuepusha shida afya ya akili

MWAKA unapomalizika tahadhari za kiafya ni muhimu kuzizingatia na kufahamu cha kufanya ili kujiepusha na magonjwa mbalimbali mojawapo ni tatizo la sasa la afya ya akili.

Wapo wengi wenye changamoto hiyo na mwanzo wa mambo hayo ni matokeo ya athari mbaya kwenye ubongo. Kumbuka kulinda ubongo na kuutunza.

BBC inajadili tabia 11 zinazoharibu ubongo wako na jinsi ya kuzishinda.

Ni taarifa zinazokusanywa kutoka kwenye ripoti mbalimbali za utafiti, zikiwamo za Shule ya Kitabibu ya Harvard na Taasisi ya Kitaifa ya Marekani ya Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu na Kiharusi (Neurological and Stroke).

Kuna mengi ya kuzingatia na ya kuepuka kuanzia ulaji na utendaji mzima wa maisha ya kila siku mojawapo ni:

KUKOSA USINGIZI

Usingizi usio wa kutosha, unatajwa na Kituo cha Sayansi ya Mfumo wa Mishipa ya Fahamu cha Marekani kuwa uharibifu mkubwa zaidi kwa ubongo unasababishwa na kukosa usingizi wa kutosha.

Usingizi wa kutosha kwa watu wazima unamaanisha saa saba hadi nane za usingizi kati ya saa 24 kwa siku. Wataalamu wanasema kuwa kulala mfululizo usiku ni bora zaidi.

Ubongo hupumzika baada ya kulala. Pia, huunda seli mpya wakati huo. Lakini ikiwa unalala chini ya saa saba, seli mpya haziundwi.

Hatimaye, haukumbuki chochote. Unapata ugumu wa kuzingatia, wa kufanya maamuzi. Kukosa usingizi huongeza shida ya akili.

Ikiwa unataka kulinda ubongo wako, kuna suluhisho moja. Pata angalau saa saba za kulala kila usiku. Japo saa nane za kulala ni bora zaidi.

Ili kufanya hivyo, unahitaji kwenda kulala angalau saa moja kabla ya kusingiza. Usitumie kifaa chochote wakati huo.

Safisha chumba cha kulala kabla ili kuunda mazingira ya usingizi. Punguza mwanga ndani ya chumba weka kila kitu vizuri.

Usilale na kufunika uso ni kwa sababu utazuia mwili kupokea oksijeni na kutoa kaboni kupitia pua.

Ukijifunika unaweza kusababisha kaboni kujilimbikiza karibu na uso matokeo yake ni uwezekano wa ukosefu wa oksijeni ukiwa usingizini.



Kupata kifungua kinywa ni muhimu, ndicho chakula cha kwanza kuupa mwili nishati ya kuendesha ubongo. **PICHA: MTANDAO**

**KIFUNGUA KINYWA**

Kumbuka hujala usiku kucha, kifungua kinywa lazima uanze nacho. Kunywa chai na vitafunio kwa sababu hutoa nishati ya kufanya kazi siku nzima.

Kuacha kifungua kinywa kunapunguza viwango vya sukari kwenye damu, jambo ambalo huathiri ubongo.

Kutopata kifungua kinywa siku baada ya siku husababisha uharibifu wa ubongo, hupunguza ufanisi wa seli.

Ukosefu wa virutubisho hufanya iwe vigumu kwa ubongo kufanya kazi kwa kawaida.

**KUTOKUNYWA MAJI**

Asilimia 75 ya ubongo ni maji ili kuweka ubongo katika hali ya unyevu maji ni muhimu sana kwa utendaji kazi wake bora.

Ukosefu wa maji husababisha tishu za ubongo kupungua na seli kushindwa kazi, hali hiyo inaweza kupunguza uwezo wa kufikiri kimantiki au kufanya maamuzi.

Kwa mujibu wa wataalamu, mtu mzima anapaswa kunywa angalau lita mbili za maji kila siku kudumisha afya ya ubongo.

Unywaji maji unaweza kuongezeka kulingana na uzito, afya, umri, mtindo wa maisha na hali ya hewa.

**KUENDEKEZA MSONGO**

Kuwa na msongo wa mawazo wa hali ya juu na wa muda mrefu husababisha seli za ubongo kufa na sehemu ya mbele ya ubongo kusinyaa. Inaathiri kumbukumbu na uwezo wa watu kufikiria.

Kulingana na watafiti, watu ambao wamezama kila wakati katika kazi. Hawawezi kusema 'hapana' kwa wengine ikiwa watatakiwa wafanye jambo fulani. Watu kama hao wanakabiliwa na mafadhaiko zaidi.

Lakini acha kufanya hivyo, epuka kuchukua mzigo wa ziada kwa njia yoyote.

Hata wanapokuwa wagonjwa, watu wengine huendelea kufanya kazi za kuushughulisha ubongo, vinginevyo, utafiti umebaini kuwa ina athari mbaya za muda mrefu kwenye ubongo.

Kukaa katika sehemu moja kwa muda mrefu kunaweza kusababisha msongo zaidi.

Mbali na hayo, kukaa nyumbani hata siku za likizo ni jambo jema.

Kutofanya harakati za kutosha au kazi za mikono, inaongeza hatari ya ugonjwa wa moyo na kisukari na tatizo la afya ya akil.

Kwa hiyo ili kuweka ubongo wenye afya, fanya mazoezi ya kawaida, uinuke kutoka kwenye kiti chako kila nusu saa, unaweza kuweka saa ya kengele kwa ajili ya hiyo, kimbia au tembea kwa nusu saa angalau siku tatu kwa wiki.

**ULEVI TEKNOLOJIA**

Kama unavyoweza kukumbuka, kizazi kilichotangulia mara nyingi kilifanya hesabu ndogo bila kutumia vikokotoo. Kilikuwa kinakumbuka namba nyingi za simu, majina ya watu, visa mikasa na hadithi tele. Leo ni tofauti.

Tabia hizi ni kama mazoezi ya ubongo, ambayo huweka nguvu zake za kufikiri na kumbukumbu imara kwa muda mrefu.

Lakini katika zama hizi huhitaji kukumbuka sana, unatumia zaidi teknolojia na hasa 'Google' hilo limepunguza uwezo wa ubongo kufanyika.

Kumbukumbu na uwezo wa kufikiri unazidi kuwa dhaifu siku baada ya siku.

Ungependa kuuweka ubongo wako katika hali ya kuchangamka, kumbuka mambo bila kutumia Google, watafiti wanapendekeza.

Unatakiwa kucheza michezo tofauti kushughulisha ubongo. Kama mafumbo.

***BBC***

***ITAENDELEA WIKI IJAYO***

# KUMBUKA MWAKA HAUBADILISHI CHOCHOTE NI WEWE UNAYEBADILISHA FIKRA ZAKO, ANZA UPYA

**INATOKA UK.11**

mia changamoto ya chuki ya baba yenu kuwa fursa ya kujisomesha na kujiongezea kipato na kusonga mbele.

Acheni kulaumu watu au marafiki kuwa ndicho chanzo cha matatizo badili fikra ili uone maisha katika sura nyingine.

**KUWA NA SHUKRANI**

Kumbuka kumshukuru Mungu. Bila kujali imani au dini yako fahamu kuwa unaishi kwa sababu kuna Mungu aliyekupa uhai na umshukuru . Unaishi kwa nguvu zake. Pia ni lazima na muhimu hapo uwashukuru watu wanaokusaidia kuendelea na mapambano ya kila siku.

Elewa umepata mafanikio 2024 kwa sababu ya nguvu za Mungu. Fahamu baraka ulizo nazo siyo kila mmoja anazo, hata afya uliyo nayo sio kwamba kila mtu ameipata.

Sio kila mtu anaishi, mamia hawana pumzi kumbuka afya uliyo nayo si Watanzania wote wanayo. Watu wangapi wamefariki unaowajua na hata usiowafahamu uliowasoma kwenye mitandao? Mambo mengi uliyo nayo mfano ujuzi na elimu ulio nayo kuna mamia wanaitafuta.

Kadhalika familia uliyojaliwa mshukuru Mungu si kulalamika eti una watoto wasichana wakati unataka wa kiume, usifikiri kutafuta nyumba ndogo mshukuru Mungu, maana wapo ambao hawana watoto.

ACHA KUJIDHARAU

Watu wanajidharau mimi sina hiki wala kile. Wanatamani au kujilinganisha na wengine. Usijidharau kwa kuangalia mafanikio ya wengine. Usiwe na dharau kwa baraka ambazo Mungu amekupa badala ya kuangalia zile ambazo huna mfano gari, nyumba, ardhi na fedha.

Kama hujafanikiwa azimia kupata mafanikio mwaka huu.

**KUMBUKA**

Mwaka mpya umenza na unatakiwa kubalisha fikra ziwe tofauti, maana majira na wakati havibadiliki ila wakubadilika ni wewe.

Unapochana kalenda ya mwaka jana, anza kwa kujishukuru na kufurahia mafanikio yako . Hata kama umenunua na kuweka kitasa kipya kwenye mlango ni mafanikio yafurahie. Usijilaumu, unajiongezea msongo, hofu na matatizo ya akili.

Kula kwa afya siyo kujaza tumbo kwa kubugia chochote ali mradi umekula. Mfano kujaza tumbo kwa ugali mkubwa na rojo la nyanya zilizoharibika au masalo siyo kujali afya. Na kupata chakula angalau mara tatu kwa siku.

Ni vizuri kufanya mazoezi, kulala muda wa kutosha, kujikinga na maradhi siyo kujiachia mfano hunawi mikono na maji tiririka kabla ya kula, unaparamia matunda sokoni bila kuosha. Kunywa pombe muda wote.

Lala kwenye chandarua kujikinga na malaria na kwenda hospitalini kama unaumwa, usikimbilie vidonge kwenye maduka ya dawa.

Usisahau kujipenda vaa vizuri na nguo safi. Tunza mwili wako na pumzika kama unaumwa maana kazi haziishi. Zipo kila siku.

Katika maisha jambo muhimu ni kukaa karibu na watu unaowapenda na kufurahi pamoja nao. Ipende familia yako na mara nyingi fanya mambo mema, saidia wenye shida au wahitaji , kucheka ni vizuri pia usisahau kujadiliana na wenzake masuala muhimu yanayohitaji ufumbuzi.

Kusali ni lazima. Jipe wakati kutafakari maisha yako na mwenendo mzima unaoupitia. Ni vizuri pia kusema hapana kama jambo hukubaliani nalo. Kadhalika ndiyo kama unaona unaridhishwa nalo.

ELIMU

NA RESTUTA JAMES

WASOMI WAAMBIWA

# Kukariri nadharia pekee hakutoshi wajue udereva, lugha nyingi na uthubutu

ELIMU ya darasani pekee haitoshi kumletea mafanikio mhitimu wa chuo kikuu, anahitaji vitu vingine hasa nidhamu ya muda na kazi, ujuzi wa ziada, uthubutu na ubunifu ambavyo ni nyenzo muhimu katika ulimwengu wa ajira.

Utafiti wa mashirika ya elimu mara kadhaa unabaini kuwa upungufu uliopo kwa baadhi ya watoto wanaohitimu elimu ya msingi hasa kutojua kusoma kwa ufasaha na kuhesabu, vyuoni hali ni tofauti, wahitimu wanakosa ujuzi mdogo ambao ungewawezesha kuogolea kwenye soko la ajira.

Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Ushirika cha Wajasiriamali Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUGECO), Revocatus Kimario, anasema moja ya pengo lililopo kwa wahitimu wa vyuo vikuu ni kutokuwa na uwezo wa kupambanua mambo hasa kutatua changamoto ndogo zinazowazunguka.

Ni ujumbe unaosikika wakati wa kuwaaga wanafunzi wanaokwenda kwenye mafunzo ya utarajali katika mataifa mbalimbali.


Anasema vijana hawajui lugha za kimataifa, udereva, elimu ya fedha na ujasiriamali, ujuzi ambao anasema unatanua fursa zao kuajiriwa na kujiajiri.

"Kuna mapengo mengi na hili nimelisema mara nyingi. Vijana hawa hawana uthubutu na uwezo wa kufanya tathmini. Kuna utafiti umetoka karibuni unaonesha kwamba asilimia 69 ya wahitimu hawana uwezo wa kuchambua kitu. Hili ni tatizo kubwa mno," anasema.

Kimario anaeleza kuwa baada ya kuona pengo hilo, ushirika huo ambao unapeleka mamia ya vijana kwenye ajira za muda mfupi nje ya nchi, unawapa ujuzi huo wa kuchambua.

"Tumesema lazima tuwafundishe biashara ili waifahamu na waweze kuona fursa na kuitumia elimu yao ya chuo kikuu kujiajiri na wengine kuajiriwa, ujasiriamali, elimu ya fedha na kuwapa nafasi ya kutekeleza kile wanachokijua. La tatu na kubwa zaidi ni hizi programu za utarajali (internship), ili wakienda nje ya nchi wapate maarifa ya teknolojia na utendaji kwa ujumla," anasema Kimario.

Anasema vijana wengi wanaopata fursa ya kufanyakazi nje ya nchi na wa sekta za kilimo na mifugo, wakiwamo madaktari wa mifugo, sayansi ya mimea na chakula, teknolojia na utalii, kilimo cha bustani na madawa, ambao wanalazimika pia




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, akiwa na baadhi ya vijana wanaokwenda kufanyakazi nje ya nchi kwa mfumo wa utarajali. **PICHA: REST JAMES**

kujua lugha za kigeni.

Kimario anatoa mfano kwamba mwaka jana, vijana 360 walishindwa kwenda Ujerumani kwa kuwa hawajui Kijerumani.

"Shida siyo maarifa. Wanakosa yale ya ziada yanayohitajika. Viwanda vya wenzetu vinatumia mashine za kisasa zilizo kwenye lugha ya Kijerumani. Wanahitaji wanaojua walau ngazi ya kwanza ya lugha hiyo," anasema.

Anaongeza: "Wanakwenda kuongeza maarifa, kuiona dunia na namna watu wengine wanavyofanya kazi na kutengeneza kipato. Tunawaambia unakwenda, 'unakopi, unaediti na unapest'." Akimaanisha

Kimario anashauri kwamba vyuo vikuu viongeze masomo ya ziada hasa ya lugha ili wanafunzi wapate urahisi wa kujifunza.

"Tukibaki tu na Kiswahili chetu tunabaki hapa ndani wakati sisi tunataka tuende huko duniani tukapanue uwezo wa vijana wetu. Ningetamani vyuo viwe na maabara za lugha au language lab," anasema Kimario.

Pengo la lugha linaungwa mkono na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, ambaye anasema ni muhimu vijana wakajua lugha za kimataifa bila kujali kozi mahsusi anayosoma chuoni.

"Nataka nieleze hili kwa masikitiko makubwa sana. Zimewahi kutoka nafasi za madereva wanaotakiwa kwenda kufanya kazi katika nchi za Ghuba mataifa ya Kiarabu, ambazo wengi walijitokeza lakini walichukuliwa wachache kwa sababu ya kutojua lugha ya Kiarabu. Tutaendelea kushirikiana na wadau ili kuona kama vyuo vinaweza kutenga muda wa ziada kwa ajili ya lugha," anasema.

Kimario anasema wanafunzi wanaopata fursa hizo ni wa vyuo vikuu na wale wa vyuo vya kati, ambapo kwa mwaka jana vijana 535 wamekwenda Ujerumani, Norway, Denmark na Sweden.

Anasema lengo hilo ni kutengeneza watu wenye ujuzi wa kutosha katika sekta ya kilimo na mifugo, ukiwamo usindakaji wa vyakula kama nyama na maziwa.

"Wanakwenda kwenye teknolojia nyingi ambazo zimetuzidi, wanapata ujuzi na kipato. Kwa wastani hawa wanaokwenda wanapata Yuro 2,500 hadi 3,000 kwa mwezi ambazo ni karibu Sh. milioni sita mpaka tisa. Wakiwa na nidhamu ya fedha, ndani ya mwaka mmoja na nusu wanaokaa kule, wanaweza kupata mtaji wa kujiajiri hapa nyumbani ," anaeleza.

Anasema elimu ya fedha waliyopewa inawawezesha kufungua akaunti ya diyaspora ili waweze kutunza fedha kwenye benki za ndani na hivyo kuiwezesha nchi kuwa na fedha za kigeni.

Anasema taarifa ya fedha ya mwaka jana, inaonesha kwamba kwenye ajira (remittance), kulikuwa na mzunguko wa dola za Marekani bilioni 625 duniani, ambazo dola bilioni bilioni 125, zilikwenda India na Afrika Mashariki, Kenya iliingiza bilioni 4.1, ambazo zilirudi nchini humo kupitia Wakenya wanaofanya kazi nje.

"Kwenye data hizo, nchi yetu ilipata dola bilioni 0.316, naamini tukishirikiana na benki tunaweza kupata mzunguko mkubwa wa fedha za kigeni. Tunaweza kupata remittance kubwa kama vijana wetu watatumia vizuri muda wao wa ziada vyuoni, kupata ujuzi wa ziada ili waweze kufanya kazi nje na nchi kuweka mifumo sahihi ya kuwawezesha," anasema.

Anatoa rai kwa serikali kuwatambua vijana waliopata mafunzo hayo na kuandaa mpango wa baada ya utarajali nje ya nchi.

Anasema SUGECO inashirikiana na Taasisi ya CRDB, kuwawezesha kimtaji, waliomaliza utarajali nje ya nchi.

"Zaidi ya vijana 40 wamewezeshwa kwa kupewa mtaji unaozidi Sh. milioni 460 ndani ya mwaka mmoja na biashara zao zinafanya vizuri. Tuna nafasi zaidi ya 1,500 za vijana kwa mwaka. Tunaamini tunaweza kutengeneza biashara nyingi zaidi, tutaongeza mzunguko wa fedha za kigeni kupitia akaunti ya diaspora na kutengeneza rasilimali watu yenye ujuzi mkubwa," anasema.

Anasisistiza umuhimu wa vijana kujifunza walau lugha mbili za kimataifa, bila kujali kozi anayosoma chuoni, kwa kuwa ni nyenzo ya mawasiliano kwa wale wanaofikiria kwenda kufanya kazi nje ya nchi.

Kimario anatoa mfano kwamba amekuwa akipeleka wanafunzi na wahitimu wa vyuo vikuu kufanyakazi katika nchi za Ulaya na Marekani na changamoto kubwa inayomkabili ni wahitimu kutojua lugha na kushindwa kuendesha gari.

Kwa mujibu wa Kimario, nchi ambazo ushirika huo unapeleka wafanyakazi ni Ujerumani, Denmark, Marekani, Uholanzi, Sweden, Norway na Israel.

Anasema mwaka jana SUGECO ilipeleka vijana 500, lakini zaidi ya nafasi 300 zilipotea kutokana na wahitimu hao kutojua Kijerumani.

Waziri Ridhiwani akiwafunda vijana hao kuwa weledi na bidii ya kazi, wanapokuwa nje ya nchi kuwaongezea fursa vijana wengine kupata mafunzo hayo.

Anawataka vijana kujiepusha na uhalifu ili wasiharibu taswira ya Tanzania ughaibuni.

"Serikali itashirikiana na SUGECO kuandaa mpango wa baada ya utarajali, ili vijana hawa waweze kutumia mafunzo waliyoyapata katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu," anasema.

Anasema maandalizi ya rasilimali watu wenye ujuzi, yanahitaji ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na taasisi mbalimbali.

Mhitimu wa SUA, Harold Mulugu, ambaye amepata fursa ya kwenda Ujerumani, anasema amelazimika kujifunza Kijerumani kwa kuwa ni moja ya kigezo cha kufanya kazi nchini humo.

Levina Kiwango ambaye amehitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kozi ya sayansi ya chakula na teknolojia, anasema amelazimika kujifunza Kijerumani baada ya kubaini kwamba ili kufikia soko la ajira nchini humo, inahitaji ajue lugha hiyo.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Wenye ushawishi mkubwa 2024

RAIS Samia Suluhu Hassan, hana mpinzani kwenye umaarufu. Ni kiongozi wa kwanza mwanamama kuongoza Tanzania na hata nchi za Afrika Mashariki.

Kinachompa umaarufu na mvuto ni msimamo wake au yale anayoyasimamia na vipaumbele vyake ni pamoja na maridhiano ya kisiasa.

Ni championi wa kuhifadhi mazingira hasa kuachana na nishati chafu ya kuni na mkaa jikoni, akifanya kampeni Tanzania na nje ya mipaka.

Anapambana na rushwa akihimiza viongozi waadilifu na msisitizo wake wa kuwa na Tanzania yenye usawa wa kijinsia pamoja na kuboresha elimu ya mwanamke bila kusahau mabadiliko ya kiuchumi na uwekezaji zaidi vinampa sifa.

Katika maeneo mengi anatajwa kama 'Mama'. Mathalani , kwenye kandanda kuna 'goli la Mama' , timu zinazoshindana mashindano ya kimataifa zikipata goli Rais, anawapa motisha ya Sh 5,000,000.



Mchungaji Boniface Mwamposa.



Ruth Zaipuna



Nape Nnauye

**MCHUNGAJI 'MWAMPOSA'**

Boniface Mwamposa ni mtu anayefahamika zaidi mwaka huu. Akijiita Bulldozer ni mchungaji anayependwa na kuaminiwa na mamilioni ya wafuasi wake na wengine wasio wa kanisa lake.

Mchungaji huyo anatoa mahubiri kwa njia ya televisheni , redio na majarida amezidi kuwa maarufu sana, akiongoza Kanisa liitwalo Arise and Shine ambalo chini ya uongozi wake huduma yake imekuwa kwa kiwango kikubwa, na kuvuta wengi

Mwamposa anashawishi mkubwa, anafahamika bila kujali imani ya dini. Anafuatwa na mamia ya watu kutoka mikoa mbalimbali wakitafuta uponyaji na pia wanamuamini kuwa anaweza kufanya jambo na kubadili maisha yao.

Kanisa hufurika waamini kila siku na mkesha wa kumaliza mwaka wa Vuka na Chako na mingine kama Vuka Kabla hujavuka ni mambo yanayovuta watu wengi kuwa sehemu ya kusanyiko lake.

**TUNDU LISSU**

Tundu Lissu ni miongoni mwa watu ambao wanazidi kuwa na ushawishi mkubwa miongoni mwa Watanzania. Wengi wanafuatilia mambo yake kwenye mitandao ya mawasiliano, vyombo vya habari , hotuba na harakati zake kisiasa. Hata kile anachosema watu wanakinukuu kwenye vijiwe mitaani.

Umaarufu wa Lissu na ushawishi wake ni ule ambao hautokani na mamlaka za pengine hasa kuwa na cheo bali ni kutokana kazi anazofanya za kimkakati za kuchochea mabadiliko hasa ya kisiasa na kuondoa hofu na woga miongoni mwa Watanzania.

Ali Kamwe na Ahmed Ally nao ni maarufu, wanasikika na kufuatiliwa kila siku. Ni wasemaji wa Simba na Yanga wanaozungumza kila wakati kuhusu timu hizo.


Misemo yao mfano Ali Kamwe anasema "gusa achia" akimaanisha Yanga inavyocheza.

Wakati Ahmed Ally ni mwasisi wa kauli mbiu ya Simba ya 'ubaya ubwela,' asili yake Kizaramo ubaya umerejea na kwamba Simba imerudi kwenye ubora wake na ina kasi mpya.

Ruth Zaipuna ni Ofisa Mtendaji Mkuu au Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, amekuwa mtendaji kwa miaka mine sasa akianza tangu Julai 2020

Yeye ndiye mwanamke wa kwanza Mtanzania kuiongoza benki hiyo akishikilia nafasi hii, ambayo anawajibika kwa wateja wa benki, wanahisa ikiwamo serikali, watu binafsi na wengine wa nje na ndani ya Tanzania.

Dorothy Semu ni mmoja wa wanasiasa machachari wanawake akiwa mwanamama anayeongoza ACT Wazalendo,



Asimwe Novath.

aliwabwaga wanaume kadhaa walokuwa wakisaka nafasi hiyo.

Anaongeza kukuru kakara za kisiasa kwenye upinzani, akitoa changamoto, maelekezo na kutaka kuwa na Tanzania mpya inayolinda na kudumisha demokrasia.

Anasisitiza na kukosoa, kwa mfano uchaguzi wa serikali za mitaa wa Novemba 2024 urudiwe maana haukuwa huru na haki.

**YALIYOTIKISA ZAIDI**

Ni kauli ya Nape Nnauye aliyesema:"Matokeo ya kura si lazima yawe yale ya kwenye boksi. Inategemea nani anayehesabu na kutangaza matokeo. Na kuna mbinu nyingi, kuna halali, kuna nusu halali na kuna haramu. Na zote zinaweza kutumika, ilimaradi tu ukishamaliza, unamwambia Mwenyezi Mungu nisamehe pale nilipokosea," anawaambia wafanyabiashara katika soko la Kashai mjini Bukoba mkoani Kagera.

Habari mpasuko anayotoa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, wakati huo kabla ya kutumbuliwa aliibua mijadala baada ya kueleweka kuwa si lazima CCM ishinde kwenye boksi la kura bali zipo mbinu nyingine haramu.

Ilikuwa Julai mwaka huu akiwa katika soko la Kashai itakumbukwa kuwa Juni 2015, mkoani Mwanza alisema CCM itashinda hata kwa bao la mkono.

Anayasema hayo miezi mine kabla ya kufanyika uchaguzi wa serikali za mitaa uliolalamikiwa na upinzania kuwa ulijaa figisu.

**MATUKIO YALIYOUMIZA**

Mwaka unapoondoka mauaji ya kinyama ya mtoto Asimwe Novath mwenye ualibino yalihuzunisha wengi kuanzia kwenye vyomba vya habari, mitandao ya kijamii, vyombo vya usafiri hadi kwenye vijiwe mitaani.

Uchungu ulizidi zaidi kutokana na baadhi ya wauaji kudaiwa kuwa ni baba yake mzazi na pia yupo kiongozi wa kanisa anayetuhumiwa kupanga na kugharamia mauaji hayo.

Alifariki Mei mwaka huu nyumbani kwao Kamachumu mkoani Kagera.

Septemba mwaka huu Ally Mohamed Kibao, alishushwa kutoka kwenye basi la Tashrif jijini Dar es Salaam wakati likielekea Tanga na kuchukuliwa na watu wasiofahamika walikuwa na pingu na silaha. Baadaye mwili wake ulipatikana Ununio Dar es Salaam.





# Chanzo cha mafuriko Dodoma chatajwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kuacha tabia ya kutupa taka ovyo kwenye mifereji ya kupitishia maji taka, kwa sababu imekuwa ni sehemu ya chanzo cha mafuriko kwenye makazi.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Edward Lemelo, alitoa ushauri huo jana wakati alipokuwa akizungumza na Nipashe jijini hapa.

Lemelo alisema wananchi wanapaswa kuacha tabia ya kutupa taka kwenye mifereji ya maji katika maeneo yao kwa sababu imekuwa ni chanzo cha mafuriko.

Alisema TARURA ilibaini kuwa kuna baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kutupa taka kwenye mifereji na kusababisha maji kuelekea kwenye makazi ya watu.

"Serikali tumejitahidi kujenga miundombinu ya mifereji hiyo kwa lengo la kulinda usalama wa wananchi na barabara lakini kuna watu wachache wanaiharibu," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo maji yamekuwa yakichangia kuharibu miundombinu ya barabara iliyojengwa. Alisema, wamekuwa wakishirikiana na viongozi wengine kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kulinda miundombinu ya barabara.

Aidha, alisema TARURA Mkoa wa Dodoma wamejipanga kuendelea kutengeneza barabara zinazoharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Alisema: "Kwa sehemu zilizoharibika sana na mvua tumekuwa tukizifanyia matengenezo ya muda ili kurudisha huduma za usafiri kwenye maeneo hayo".

Vile vile, alisema wamepanga kila wilaya kuhakikisha barabara zote zinazoharibiwa na mvua zinafanyiwa matengenezo haraka.

Alisema: "Maeneo ya Wilaya ya Kondoa Vijijini yaliathirika na mafuriko ya mvua lakini hivi sasa tumerudisha huduma ya usafiri kwa sababu barabara ni uchumi, hivyo zinatakiwa kulindwa ili shughuli za maendeleo zifanyike kila siku".

# Askofu 'awang'ata' sikio viongozi CHADEMA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Baptist Tanzania Kanda ya Kati, Antony Mlyashimba, amesema viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), waache kuishi kwa mazoea bali wafuate katiba yao inavyoelekeza.

Alitoa ushauri huo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mvutano uliopo hivi sasa ndani ya chama hicho kuelekea uchaguzi wa mwenyekiti wao.

Alisema kuendelea kuvutana na kutoleana maneno kwa viongozi wakuu wa chama hicho kunakidhoofisha chama chao, kwamba wanachopaswa kufanya ni kufuata katiba badala ya kurushiana maneno kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

"Hichi kinachofanyika hivi sasa kwa viongozi wakuu wa chama kurushiana maneno siyo jambo jema kwa chama kwani kinadhoofisha chama na kutoa mwanya kwa vyama vingine kupata nafasi ya kujua madhaifu yao," alisema na kuongeza:

"Leo hii ndani ya chama kuna baadhi ya viongozi wakuu wa chama wanadai kuwa Lissu ni mlopokaji hafai kuwa kiongozi, lakini wengine wanasema Mbowe hataki kuachia kiti lakini pia anatumia vibaya madaraka yake hii yote ni sehemu ya kukidhoofisha chama ni sawa ni kuvuana nguo," alisema.

Alisema ili kuondokana na hali hiyo, CHADEMA wanapaswa kuishi kwa mujibu wa Katiba yao na kuacha mazoea ya nani anapaswa kuwa kiongozi na nani hapaswi.

"Mimi ningewashauri kufuata katiba yao tuu inasemaje kama kuna mtu anasifa ya kugombea agombee kwa mujibu wa Katiba yao na kuwaacha wanachama kuamua nani kuwa kiongozi wao badala ya kuendelea kuzozana kama ambavyo walivyokuwa wanafanya hivi karibuni hali ambayo kwa kiasi kikubwa inaweza kukidhoofisha chama chao," alisema Askofu Mlyashimba.

Hata hivyo, alisema Tanzania bado inahitaji uwepo wa chama cha upinzani chenye nguvu ambacho kitasaidia kuikosoa serikali iliyoko madarakani kwenye upungufu mbalimbali wa kiutawala.



Vifaa vya kuhifadhia taka vikionekana kuchakaa kutokana na kukaa kwa muda mrefu bila kubadilishwa vilivyowekwa katika eneo la Mlezi jijini Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vijana waitwa kufuga nyuki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

VIJANA wametakiwa kuitumia misitu kwenye shughuli za ufugaji nyuki badala ya kupoteza muda kutembea mijini na barua za kuomba kazi, jambo ambalo linawachelewesha kufikia malengo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kijiji cha Nyuki, Philemon Kiemi, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wanafunzi waliosoma katika Shule ya Sekondari ya Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida kuanzia 1991-1994.

Alisema hivi sasa ajira serikalini ni ngumu hivyo vijana wanapaswa kutumia fursa hiyo ya msitu iliyopo nchini kwenye ufugaji nyuki.

"Vijana wanaotembea na barua katika miji kama Dodoma, Dar es Salaam, Arusha na maeneo mengine nawashauri watembelee misitu waione fursa, waone misitu kama ofisi badala ya kutembea na barua kutafuta kazi huko ni kupoteza muda," alisema.

Kiemi ambaye ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) mwaka 2012, alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2024 watalii zaidi ya 6,000 wametembelea kijiji cha nyuki kufanya utalii na kujifunza ufugaji wa nyuki ambapo kati ya hao 1,700 wametoka nje ya nchi.

Alisema katika kipindi hicho wananchi zaidi ya 4,800 kutoka katika vijiji na kata zote za Mkoa wa Singida wamepewa mafunzo ya ufugaji nyuki na vifaa vinavyotumika katika ufugaji huo ikiwamo mizinga hatua ambayo itaongeza uzalisha wa mazao ya nyuki hususani vumbi la Singida.

"Naishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ambayo yametuwezesha sisi vijana kuingia kwenye biashara ya ufugaji nyuki na kujipatia kipato ambapo mazao yatokanayo na nyuki yanapata soko vizuri ndani na nje ya nchi," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi waliosoma Shule ya Sekondari ya Mwenge, Emmanuel Hanai, alisema uwekezaji uliofanyika katika kijiji cha nyuki ni mzuri na unavutia watu wengi kwenda kutembelea na kujifunza.

Hanai ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Washauri Elekezi wa Mazingira Tanzania (TEEA), alisema serikali itie mkono kuwasaidia vijana waliojikita katika biashara ya ufugaji nyuki kwa kuhakikisha mazao yanazalishwa yanapata soko ndani na nje ya nchi ili kuinua uchumi wao.





# Wananchi kata tano Lupembe wapata huduma 'ambulance'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI kutoka kata tano za Lupembe wilayani Njombe, wanatarajia kuondokana na adha ya kukodi usafiri kwa gharama kubwa pamoja wajawazito kupanda bodaboda wanapofuata huduma hospitalini, baada ya serikali kuwaletea gari la kubebea wagonjwa.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kukabidhiwa gari hilo katika Kituo cha Afya Mtwango na Mbunge wa Lupembe, Edwin Swalle wananchi hao walisema wanaishukuru serikali na mbunge huyo kwa kutatua kero hiyo.

Sara Kaduma alisema wanafuraha kwa kuletewa gari la wagonjwa kwa ajili ya kuwawezesha usafiri pindi wanapopewa rufaa ya kufuata matibabu katika maeneo mengine.

"Ni kweli hospitali zipo, vituo vya afya vipo lakini pindi tunapotakiwa kwenda mbele zaidi labda mtu anatakiwa kujifungua anapandishwa kwenye boda boda mpaka anafika hospitali mtoto anakuwa amepata changamoto kwa hiyo vifo vingi vya watoto vimetokea," alisema Sara.

Naye Shabani Kiduga alisema uwepo wa gari hilo kutawasaidia kuwapeleka wagonjwa katika hospitali za rufani ikiwemo mkoani Mbeya au Njombe.

"Huko nyuma tulikuwa tunapanda magari ya abiria au boda boda hali ambayo ilikuwa ni hatari kwa mgonjwa pamoja na kulipa gharama kubwa, tunamshukuru sana mbunge wetu pamoja na serikali kwa kutuletea gari hili tumefurahi sana," alisema Kiduga.

Awali Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Edwin Swalle alisema gari hilo linakwenda kuwaondolea wananchi adha kwa kiasi kikubwa na kueleza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan amewapendelea kwa kutatua changamoto za afya katika jimbo hilo.

Swalle alisema wajawazito wengi wamepoteza maisha kutokana na kukosekana gari la wagonjwa kwa ajili ya kuwapeleka katika hospitali kubwa.

"Hili gari limekuja kuwa mkombozi, Rais Samia ametukomboa na tumelipokea kwa heshima na tutamuomba tena atuongezee magari mengine kwa sababu Kata ya Kichiwa pia kuna kituo cha afya," alisema Swalle.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli alishukuru kwa kuletewa gari hilo na kueleza kuwa mbunge huyo amekuwa akifanya maendeleo bila ya kuangalia ukanda.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Christopher Sanga alisema walikuwa na kata tano ambazo zilikuwa zinakosa huduma ya gari la wagonjwa na kwamba uwepo wa gari hilo litasaidia wananchi kuondokana na adha hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mtwango, Beno Makero alisema walikuwa wanapata shida kwa sababu ya kukosekana kwa gari ya kubebea wagonjwa hivyo wakati mwingine walilazimika kukodi gari za watu binafsi ili kuwapeleka wagonjwa kwenye hospitali kubwa.




Mkurugenzi wa Shirika la Tree of Hope la jijini Tanga, Fortunata Manyeresa, akizungumza na wakazi wa kijiji cha Msomera kilichoko wilayani Handeni mkoani Tanga jana, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakazi wa kijiji hicho kuhusu ukatili wa kijinsia na kujenga ustahimilivu wa jamii katika kukabiliana na athari za tabianchi. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## TRA yawaita wa'biashara ukadiriaji kodi 2025

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYABIASHARA mkoani Njombe wametakiwa kufika kwenye ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zilizopo kwenye maeneo yao ili kukadiriwa kodi ya mwaka 2025.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe, Spaceoza Owure wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Owure aliwataka wafanyabiashara wote kuhakikisha hadi ifikapo Machi 31 mwaka 2025 wawe wamekadiriwa kodi zao.

"Tunawaomba wafanyabiashara kufika wenyewe kwenye ofisi za TRA badala ya kutuma wawakilishi ili kuondokana na migogoro isiyo na sababu," alisema Owure.

Hata hivyo meneja huyo alisema kwa mwaka 2024 lengo lilikuwa ni kukusanya Shilingi bilioni 35.817 na kuanzia Julai hadi Novemba wamekusanya Shilingi bilioni 14.155.

Aidha zoezi la ukadiriaji kodi linaanza Januari Mosi hadi Machi 31 mwaka 2025, ambapo mfanyabiashara atatakiwa kulipa kodi yake ya mwaka kwa awamu nne.

Awamu ya kwanza ya ulipaji kodi ni Januari hadi Machi, awamu ya pili ni Aprili hadi Juni, awamu ya tatu ni Julai hadi Septemba na awamu ya nne ni Oktoba hadi Desemba.

**Owure aliwataka wafanyabiashara wote kuhakikisha hadi ifikapo Machi 31 mwaka 2025 wawe wamekadiriwa kodi zao.**

# Samia achangia mil.35/- ujenzi Kanisa Anglikana

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

RAIS Samia Suluhu Hassan amechangia Sh. milioni 35 kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa la Anglikana lililopo Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe.

Mchango huo ulikabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe kwa niaba ya Rais Samia katika katika harambee iliyofanyika katika kanisa hilo kwa lengo la kukusanya Sh. milioni 310.

Mtaka alisema Rais Dk. Samia anatambua mchango wa madhehebu ya dini katika kudumisha amani na utulivu sambamba na kuwapongeza viongozi wa dini kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kusaidia maendeleo ya kijamii, ikiwemo kusimamia maadili na kuwaongoza waumini kuwa raia wema.

"Madhehebu ya dini na viongozi wa kidini mnafanya kazi kubwa sana ya kusaidia maendeleo ya nchi yetu, endeleeni kuliombea mema taifa letu na kusimamia maadili kwa waumini wenu," alisema Mtaka.

Mtaka aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu ya namna ya kukabiliana na matukio ya ukatili na udumavu ambayo yamekuwa yakiathiri familia kutokana na ndugu zao kuuawa, kubakwa na wengine kujinyonga.

Mtaka alitoa rai kwa kanisa hilo kuanza kubuni vitega uchumi vitakavyolipatia fedha kanisa kwa sababu Njombe inazo fursa nyingi ambazo bado zinapaswa kufanyiwa kazi.

"Kutokana na uhaba mkubwa wa mbegu za mazao mbalimbali ikiwemo, viazi, mahindi na mazao ya wanyama hasa samani, kuku na ng'ombe ni wajibu wakazi wa Njombe kuona namna ya kutumia fursa hiyo kwa mwaka 2025 ili kukuza uchumi wa mtu mmoja na mkoa kwa ujumla hali itakayosaidia kupunguza uagizaji wa mbegu hizo kutoka mikoa mingine," alisema Mtaka.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Tanganyika Kusini Magharibi, Mathew Mhagama alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuchangia ujenzi wa kanisa hilo.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kuwa mgeni rasmi kwenye hafla hii kupitia mwakilishi wake na kwa mchango wake wa Sh. milioni 35. Pia, tunawashukuru viongozi wote walioshiriki katika hafla hii na kuchangia, kufanikisha kupatikna Sh. milioni 60 na mchango huu utasaidia sana kukamilisha ujenzi wa kanisa letu," alisema Mhagama.

Katika harambee ya ujenzi wa kanisa hilo, zaidi ya shilingi milioni 60 zilipatikana, ahadi ikiwa ni shilingi milioni 13 na fedha taslimu ni shilingi milioni 47.84, huku mahitaji yakiwa ni Sh. milioni 310.

## Dk. Tulia ataka hatua kudhibiti wahamiaji haramu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson amelitaka Jeshi la Uhamiaji kuendelea kudhibiti wahamiaji haramu ili nchi ibaki kuwa salama na kuendelea na harakati za maendeleo.

Alitoa agizo hilo juzi visiwani hapa baada ya kuweka jiwe la msingi jengo la Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kuendelea kuishi na wageni wanaoingia kinyemela bila kufuata utaratibu wa uhamiaji ni kuiweka nchi katika hatari ya kupoteza tunu ya amani na usalama.

"Hakuna nchi inayoweza kuendelea bila ya kuwa na amani, amani ndiyo msingi wa maendeleo katika taifa lolote, bila ya amani na usalama hakuna maendeleo" alisema Dk.Tulia.

Alisema kuwa ulinzi wa taifa ni jukumu la kila mmoja na kuwataka wananchi kutowapokea wageni wasiowafahamu na kutoa taarifa za uwepo wao ili kudhibitiwa kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla.

Pia, aliishauri jamii kushirikiana na Jeshi la Uhamiaji kuendelea kupiga vita biashara ya usafirishaji wa binaadamu ili kuendelea kujikomboa katika madhila ya kutawaliwa na utumwa uliyokuwepo kabla ya Mapinduzi.

Aidha, aliwataka maofisa na wapiganaji wa Jeshi la Uhamiaji kuendelea kutoa elimu ya ulinzi wa mipaka ya nchi hasa kwa watumiaji wa bahari (wavuvi), ili kusaidia ulinzi katika maeneo hayo yanayoonekana kuwa maarufu kwa uingiaji wa wageni na usafirishaji wa binaadamu.

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Uhamiaji, Dk. Anna Makala alisema kukamilika kwa jengo hilo kutaongeza usalama wa wilaya.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Islam Seif Salum alisema jengo hilo limejumuisha eneo la mapokezi na huduma za kijamii zinazozingatia jinsia na watu wenye mahitaji maalum.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Baran Sillo, alisema katika miaka 61 ya Mapinduzi Idara ya Uhamiaji imepata mabadiliko chanya katika utendaji na miundombinu.

Alisema hadi sasa kuna majengo17 yakiwemo 15 ya makazi ya askari Unguja na Pemba na wanaendelea kutoa huduma za hati za kusafiria, visa, vibali vya ukaazi kwa wageni, kudhibiti mipaka kwa njia za kidijitali.

# Kilo 798 dawa za kulevya zakamatwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (ZDCEA) kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama imefanya operesheni maalum za kimkakati na kufanikiwa kukamata kilogramu 798.893 za dawa za kulevya.

Dawa hizo ni aina ya bangi, cocaine, heroin, methampetamine na shisha zilizochanganywa na dawa za kulevya.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Kamishna wa ZDCEA Kanal Nassoro Burhani, alisema kiwango hicho kilichokamatwa ni kikubwa ambacho hakijawahi kukamatwa katika historia ya Zanzibar tangu Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Alisema dawa hizo zingefanikiwa kuchepushwa na kuingia mtaani zinaweza kutengeneza kete milioni 27, wakati idadi ya watu wote Unguja na Pemba ni milioni 1.8 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Alisema katika operesheni hiyo gari sita, boti moja na watuhumiwa tisa kati yao nane ni raia wa Tanzania na mmoja ni raia wa kigeni, ambapo wote wamekamatwa kwa tuhuma za kuhusika na dawa hizo na baadhi yao tayari wamefikishwa mahakamani.

Alisema operesheni ya kwanza ilifanyika Oktoba 17 mwaka huu katika eneo la Bandari ya Majahazi Malindi na kufanikiwa kukamata watuhumiwa wawili Haji Suleiman Ali (18) na Mbaraka Rajab Kiee (34) wakazi wa Maungani wakiwa na dawa za kulevya aina ya bangi gramu 734.95 zilizokuwa zimefichwa katika boti.

"Taarifa fiche zinaeleza kuwa watuhumiwa hao walikuwa wanafanya biashara ya dawa za kulevya ndani ya eneo la Bandari ya Malindi katika maegesho ya majahazi. Aidha, watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani baada ya upepelezi kukamilika"alisema.

Alisema operesheni ya pili ilifanyika Novemba 5, 2024, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ambapo walifanikiwa kukamata shisha boksi 15 sawa na pisi 300 zenye uzito wa kilogramu 263 zilizoingizwa nchini kutoka China na mtuhumiwa Alperen Karakurum raia wa Uturuki.

Aidha alisema baada ya kukamatwa kwa shisha hizo zilifanyiwa uchunguzi wa kitaalamu katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na kubainika kuwa ndani yake kuna kemikali mbalimbali ikiwemo ya "bufotenin" ambazo zinapumbaza akili ya mtumiaji na kusababisha athari mbalimbali za kiafya ikiwemo magonjwa ya moyo.

Alisema operesheni ya tatu, ilifanyika Novemba 5, 2024 majira ya usiku, katika operesheni iliyofanyika eneo la Kilimani Chini na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa Ali Mohamed Ali maarufu Ali Macho, mkazi wa Mpendae akiwa na dawa za kulevya aina ya cocaine zenye uzito wa 87.223.

Aidha, katika eneo la Mtendeni walifanikiwa kumkamata mtuhumiwa Fahad Ali Khamis akiwa na dawa za kulevya aina ya cocaine zenye uzito wa gramu 111.6678.

Alisema: "Operesheni ya nne, ilifanyika Novemba 15 katika eneo la Kisauni, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi. Katika operesheni hiyo mamlaka imefanikiwa kuvuja rekodi yake ya mwezi Januari 2024, mara hii tumefanikiwa kukamata dawa za kulevya aina ya methampetamine zenye uzito wa kilogramu 536 na heroin kilogramu moja zilizokuwa zimehifadhiwa katika nyumba iliyopo eneo la Kisauni".



Mbunge wa Malindi CCM Zanzibar, Mohamed Suleiman Salumu (kulia), akiteta na Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Vijana wa jimbo hilo, Amir Mussa Amir, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuwaelimisha vijana elimu ya upigaji kura uliofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari Lumumba mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Naibu Spika aipa kongole TAWEN ufikishaji huduma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, amesema ubunifu wa Taasisi ya Tanzania Women Empowerment Network (TAWEN) kufungua matawi kila mkoa na kuwakutanisha viongozi wenye nia moja ya kupambana katika masuala ya wanawake na vijana ni jambo la kuigwa.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo, hafla iliyofanyika katika visiwani hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia serikali kutatua changamoto za wajasiriamali wanawake kwenye siasa na uchumi ambao imekuwa vigumu kuzifikia baadhi ya fursa zinazotolewa kwa ajili yao.

"Serikali inatengeneza fursa kwa wajasiriamali na wanawake lakini baadhi yao imekua vigumu kuzifikia kutokana na changamoto mbalimbali TAWEN itasaidia jambo hili," alisema.

Aidha alisema lengo la TAWEN ni kuwawezesha wanawake na vijana kutambua mchango wao, kuthibitisha misingi ya kiuchumi, kiuongozi na kitamaduni katika kutengeneza jamii ili kuleta usawa wa kimawazo na kimaendeleo.

Aidha, alisema TAWEN imedhamiria kwa vitendo kuunga mkono juhudi za serikali ikiwemo kutoa elimu na hamasa kwa wanawake na vijana kwenye masuala ya uwezeshaji kiuchumi na utuzaji wa mazingira.

Sambamba na hayo aliwataka wajasiriamali wanawake kutumia fursa ya kuzungumza mafanikio na changamoto zao ili kupeana uzoefu na njia bora za kufikia maendeleo.

Mlezi wa TAWEN, Balozi Amina Salum Ali alisema asilimia 88 ya wakazi wa Zanzibar wanatumia nishati salama ya kupikia.

Makamu Mwenyekiti TAWEN, Thuwaiba Kisasi alisema miongoni mwa majukumu yao ni kuhakikisha wanawaunganisha wajasiriamali na taasisi za kifedha ili kutumia fursa, kujinyanyua kiuchumi na kufikia maendeleo yao.

Mkurugenzi Mtendaji TAWEN Tanzania, Florence Masunga alisema TAWEN imejikita katika miradi mikubwa inayowagusa wananchi ikiwemo matumizi ya nishati safi ya kupikia na tayari imefika katika mikoa saba ya Tanzania Bara.

Alisema wamefanikiwa kugawa majiko ya gesi 1,700, na kukopesha zaidi ya majiko 3,000 yanayotumia umeme mdogo kwa lengo la kupunguza matatizo ya kupumua hasa kwa wanawake ili kuongeza uchumi wao.

# Tanzania yaimarisha uwezo wa kujenga biashara mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema inaimarisha miundombinu wezeshi na mifumo muhimu ya kufikisha kwenye makazi ya watu bidhaa zinazonunuliwa kupitia mtandao.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari alisema jana kuwa hadi Septemba walishatoa leseni 146 za huduma wezeshi za mitandao, ambao wanawezesha upatikanaji wa huduma za intaneti.

"Watumiaji waliopata huduma za intaneti kupitia vifaa vya mkononi vilivyounganishwa kwa waya na visivyounganishwa walifikia 41,376,545 kipindi hicho,"alisema na kuongeza:

"Akaunti za simu za mkononi ambazo zinawezesha malipo mtandaoni zilifikia 60,815,533 ambazo zilifanya miamala 310,881,561 katika kipindi cha Septemba mwaka huu".

Aidha, alisema serikali inasimamia mipango ya kuendeleza biashara mtandao pamoja na kuunganisha mfumo wa taifa wa anwani na postikodi (NAPS) na mifumo mingine na majukwaa ya huduma za kijamii.

"Biashara mtandao pia inategemea mifumo imara ya usafiri na usambazaji, urahisi wa kufikisha majumbani au maofisini vifaa vinavyoagizwa kidijiti unatokana na kukua kwa mawasiliano ya mkononi, matumizi ya intaneti, mitandao ya kijamii, fursa za kutangaza na kununua biashara mitandaoni na ufanisi wa mawasiliano,"alisema.


Vilevile alisema imeanzisha mpango wa kujenga maghala la kuhifadhi vitu vinavyoingia Tanzania kwa mfumo wa biashara mtandao.

Kwa mujibu wa Dk. Bakari, NAPS imebadilisha utoaji wa huduma za kiposta na usafirishaji wa vifurushi Tanzania, vifaa vinavyonunuliwa kielektroniki vinafikishwa kwa wateja kupitia anwani zinazofahamika.

"Ufikishaji huu unafanywa na watoa huduma za usafirishaji vifurushi, ambapo walio na leseni za TCRA walikuwa 147 katika kipindi cha Septemba mwaka huu, au kwa utaratibu mwingine unaohusisha magari madogo na pikikipi zinazobeba abiria (bodaboda),"alisema.

Aliongeza: "Tanzania iko kwenye nafasi nzuri sana ya kuwa kiungo muhimu cha biashara mtandao eneo hili la Afrika. Imezungukwa na nchi nane ambazo kati yake tano hazipakani na bahari. Vilevile Shirika la Ndege Tanzania linajenga uwezo wa kusafirisha mizigo kwa njia ya anga". Dk. Bakari alisema pamoja na kuwezesha utoaji wa huduma, NAPS inafanikisha shughuli za kiserikali na uendeshaji, kwamba mfumo unafanikisha mawasiliano ya serikali na wananchi.

Alisema: "Mfumo huu, unaoratibiwa na TCRA ulifanikisha sana Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Hii ilikuwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa maelekezo mahsusi ya kuuimarisha"



Ofisa Uuguzi wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Flora Zacharia, akimpima shinikizo la damu, mapigo ya moyo na kiwango cha oksijeni mwilini msanii wa muziki Zuhura Othman Soud (Zuchu) alipofika katika kliniki ya taasisi hiyo, iliyopo Kawe kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa magonjwa ya moyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JKCI**

## Ulega atoa maagizo matano ujenzi barabara Kigamboni

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega ametoa maagizo matano kwa mkandarasi anayetekeleza miradi ya ujenzi wa barabara wilayani Kigamboni, Dar es Salaam, Nyakemore Engineering Group kuhakikisha anakamilisha kwa wakati na ubora unaohitajika.

Alitoa maagizo hayo jana alipozuru katika wilaya hiyo yenye lengo la kukagua maendeleo ya miradi ya ujenzi wa barabara.

Akiwa katika eneo la Kigamboni Mnadani, Waziri Ulega alieleza kuwa barabara hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hivyo ni lazima marekebisho yake yakamilike haraka.

Hivyo, alisisitiza umuhimu wa kuhakikisha barabara haifungwi wakati wa ujenzi ili kuepusha athari kwa shughuli za kijamii na kwa wananchi wanaokwenda kufuata huduma za kijamii ikiwamo huduma za afya, masoko, ofisi za umma.

Waziri Ulega alisema: "Ni lazima barabara iwe inapitika hata wakati wa ujenzi ili wananchi waendelee kupata huduma muhimu. Tunataka kazi hii ikamilike ifikapo Januari 30, mwakani na nitakuja kukagua na kuifungua rasmi. Mkandarasi anapaswa kufanya kazi usiku na mchana, kuongeza wataalamu, vibarua, na vifaa ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na changamoto ya msongamano inatatuliwa haraka".

Aidha, Waziri Ulega aliagiza kuwekwa utaratibu wa kudhibiti kasi ya malori yanayopita katika barabara ya Kigamboni, ili kuhakikisha usalama wa watumiaji wa barabara.

Pia, alisisitiza umuhimu wa kujenga vituo vya mabasi kandokando ya barabara hiyo ili kuimarisha usafiri kwa wananchi.

Vilevile, alimwagiza mkandarasi kutumia njia za ubunifu ili kuondoa msongamano wa magari katika eneo la Kigamboni Mnadani na maeneo mengine na kuhakikisha shughuli za ujenzi haziathiri ratiba za kila siku za wakazi wa eneo hilo.

# 52 wafanyiwa upasuaji magonjwa ya macho

**Na Christina Mwakangale**

WATU 52 kati ya 405 wamefanyiwa upasuaji wa magonjwa ya macho mkoani Ruvuma ikiwamo kuondoa mtoto wa jicho, huku mmoja akipatiwa rufani ya kutibiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Upasuaji huo ulifanyika katika Hospitali ya Misheni ya Mtakatifu Joseph Peramiho kwenye kambi ya siku nne, iliyoandaliwa na MNH pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, kuanzia Desemba 26 hadi 29.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Dk. Geofrey Kihaule, alisema wananchi 27 kati ya 405, wamepatiwa miwani kutokana na kubainika wana changamoto za uoni hafifu, huku wengine wakipatiwa matibabu ya kawaida ya macho.

Dk. Kihaule aliongeza kuwa pamoja na uchunguzi na matibabu hayo, wataalamu wa Hospitali ya Peramiho wamepata fursa ya kujengewa uwezo bobezi, ili kuboresha huduma za matibabu ya magonjwa ya macho.

"Napenda kuupongeza uongozi wa MNH kwa kuona umuhimu wa kuwaleta madaktari hawa kutoa huduma katika halmashauri yetu, uamuzi huu umewapunguzia wakazi wa Songea na maeneo ya jirani umbali na gharama za kwenda Dar es Salaam (Muhimbili) kupata matibabu haya," aliongeza Dk. Kihaule.

Mmoja wa wananchi aliyehudumiwa katika kambi hiyo, Bryson Mapunda, alishukuru serikali kwa kuwajali wananchi wa Songea na kuomba utaratibu huo uendelee ili kuongeza wigo wa huduma za ubingwa bobezi.

Awali, akizindua kambi hiyo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Dk. Louis Chomboko, aliushukuru uongozi wa MNH kwa kuona umuhimu wa huduma hizo za kibingwa na kuletwa wataalamu kuungana na wenzao kutoa huduma hiyo.

Dk. Chomboko alisema: "Hatua hii itapunguza changamoto kubwa ya wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma za uchunguzi na matibabu ya macho katika mikoa mingine."

Aliongeza: "Tunaishukuru serikali kwa jitihada za kutusogezea huduma hizi karibu na wananchi. Hii inasaidia kupunguza gharama, inarahisisha wananchi kupata huduma za afya za bila kujali umbali."

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka MNH, Joachim Kilemile, alisema kuwa huduma zilizotolewa katika kambi hiyo ni uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ya macho, utoaji wa miwani na dawa kwa wenye matatizo.

Alisema pia waliohitaji upasuaji wamefanyiwa huduma hiyo papo hapo na baadhi kupata rufani.

# Jimmy Carter akumbukwa kuiweka dunia salama

**WASHINGTON, Marekani**

VIONGOZI mbalimbali duniani wamemtaja Rais wa zamani wa Marekani, Jimmy Carter, ambaye amefariki dunia jana ni mtu wa amani, mpenda haki na usawa.

Carter ambaye alikuwa Rais wa Marekani kuanzia 1977 hadi 1981, alifariki akiwa nyumbani kwake Plains akiwa na umri wa miaka 100.

Taarifa zilizotolewa na kituo cha Carter, zilisema rais huyo wa zamani alifariki akiwa amezungukwa na familia yake.

„Baba yangu alikuwa shujaa, sio kwangu tu lakini kwa kila mmoja anayeamini katika amani, haki za binadamu, na upendo usio na ubinafsi," alisema mwanawe wa kiume, Chip Carter.

„Ulimwengu ni familia yetu kwa sababu ya jinsi alivyowaleta watu pamoja, na tunakushukuru kwa kuheshimu kumbukumbu yake kwa kuendelea kufuata imani hizi za pamoja," aliongeza.

**KUFIKISHA MIAKA 100**

Kiongozi huyo kutoka Chama cha Democrat, alikuwa rais wa 39 wa Marekani, anavunja rekodi kwa kuishi muda mrefu zaidi baada ya kumaliza muhula wake madarakani kuliko mwingine yeyote wa nchi hiyo.

Katika kipindi chake cha urais, anakumbukwa kwa kuweka matukio ya kihistoria katika Mashariki ya Kati, ikiwamo kusimamia mikataba ya Amani ya Camp Dave ya mwaka 1978 kati ya Misri na Israel.

Mkataba huo ulipelekea kupatikana amani kati ya nchi hizo mbili katika mwaka wa 1979. Pia alikuwa rais wakati Marekani iliposimamia mazungumzo ya kuwachiwa huru wafanyakazi 52 waliokuwa wamezuiliwa kwenye ubalozi wa Marekani mjini Tehran nchini Iran.

Wafanyakazi hao walichukuliwa mateka baada ya Mapinduzi ya Kiislamu ya mwaka 1979 kwa siku 444.

Licha ya kushindwa kupata muhula wa pili wa urais, Carter alianzisha Kituo cha Carter ambacho kilisimamia mazungumzo hayo na kuachiwa mateka hao dakika chache baada ya kuapishwa kwa Rais Ronald Reagan mnamo 1981.

Kupitia kituo hicho, alilenga kuongoza juhudi za amani kimataifa, kutetea demokrasia, afya ya umma na haki za binadamu.

**KUZALIWA KWAKE**

Carter alikuwa rais wa kwanza wa Marekani ambaye alizaliwa hospitali, Oktoba 1, 1924 mjini Plains, katika jimbo la Georgia.

Mama yake alikuwa muuguzi na mmiliki wa duka la jumla. Baada ya maisha ya utotoni yaliyogubikwa na kipindi cha mtikisiko wa kiuchumi, alijiunga na Chuo cha Jeshi la Wanamaji na huko alikutana na rafiki wa dada yake, Rosalynn Smith, ambaye walioana 1946 na waliishi kwa miaka 77, hadi Rosalynn alipofariki Novemba 2023 akiwa na umri wa miaka 96.

**VIONGOZI WAMLILIA**

Rais anayeondoka madarakani Joe Biden, aliwaongoza marais wastaafu wa Marekani na viongozi wengine wa dunia kutuma salamu za rambirambi kufuatia kifo cha Carter.

„Marekani na ulimwengu imempoteza kiongozi wa ajabu, mzee wa taifa na mfadhili wa kibinadamu," alisema Rais Biden katika taarifa iliyotolewa na Ikulu ya White House. Katika salamu zake katika hotuba ya televisheni aliongeza kuwa Carter aliishi maisha yaliyopimwa sio kwa maneno bali kwa matendo yake.

Rais mteule Donald Trump, alisema Wamarekani wanapaswa kumlipa Carter deni la shukrani. „Changamoto ambazo Jimmy alikabiliana nazo akiwa rais zilikuja katika wakati muhimu kwa nchi yetu na alifanya kila awezalo kuboresha maisha ya Wamarekani wote," alisema kwenye mtandao wa kijamii.

Rais wa zamani wa Marekani, Bill Clinton alisema mtangulizi wake alifanya kazi bila kuchoka kwa ajili ya ulimwengu uwe bora na wa haki.

Kwa upande wa George W. Bush alisema Carter aliiheshimu ofisi. Na juhudi zake za kuwa na ulimwengu bora hazikuishia na urais.

Barack Obama alimsifu Carter kwa kufundisha kuwa maana ya kuishi maisha ya neema, heshima, haki na huduma.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, alisema Carter atakumbukwa kwa mshikamano wake na walio hatarini, neema yake ya kudumu, na imani yake isiyo na kikomo katika manufaa ya wote na ubinadamu wetu wa pamoja.

***DW***



Waokoaji wakibeba watu wawili waliokolewa kati ya 181 waliokuwa kwenye ndege iliyoanguka juzi katika Uwanja wa Ndege Muan, Korea Kusini. **PICHA: ICHAAFP**

## Rais mpya Georgia aapishwa

RAIS mpya wa Georgia, Mikheil Kavelashvili, ameapishwa rasmi jana kuongoza nchi hiyo, huku mtangulizi wake Salome Zourabichvili, akikubali kuondoka Ikulu baada ya hapo kugoma kuiachia.

Zourabichvili, ambaye anaunga mkono Umoja wa Ulaya, aliwaambia wafuasi wake kwamba anaondoka ikulu, lakini anasalia kuwa rais halali.

Awali, Zourabichvili alisisitiza kuwa katu hataondoka Ikulu akipinga ushindi wa Kavelashvili.

Kwa wiki kadhaa, maelfu ya watu walikuwa wakiandamana kila siku nchini Georgia, wakitaka kurejeshwa kwa sera zinazounga mkono Umoja wa Ulaya.

Aidha, wamekuwa wakitaka uchaguzi wa bunge uliofanyika Oktoba, ambao chama cha kizalendo kinachotawala Georgian Dream party kilichopata ushindi urudiwe.

Waandamanaji wana hofu kwamba chama hicho kina uhusiano wa karibu na Russia na kitaimarisha urafiki huo, miongo kadhaa tangu ilipojitoa kwenye muungano wa kisovieti.

Tayari chama tawala kimesimamisha mazungumzo ya nchi hiyo kujiunga na Umoja wa Ulaya hadi mwaka 2028, na kusababisha maandamano nchini humo.

**Zourabichvili, ambaye anaunga mkono Umoja wa Ulaya, aliwaambia wafuasi wake kwamba anaondoka ikulu, lakini anasalia kuwa rais halali.**

# Maandamano yanukia Kenya kupinga utekaji nyara watu

**NAIROBI, Kenya**

WANAHARAKATI wa kutetea haki za binadamu, vijana na watu walionusurika katika matukio ya utekaji nyara nchini Kenya, wametangaza kufanya maandamano Jumatatu kupinga vitendo hivyo.

Walioitisha maandamano hayo walisema maandamano hayo yatafanyika nchini kote na matayarisho yanakwenda kama yalivyopangwa katika kaunti zote 47.

Walisema kuwa maandamano hayo yanalenga kuishinikiza serikali kuwaachilia huru watu wanaoaminika kutekwa nyara, kukomesha kukamatwa kiholela kwa watu na kushughulikia madai yaliyotolewa na waandamanaji vijana wa Generation Z mwezi Juni.

Ongezeko la matukio ya utekaji nyara ya zaidi ya watu 10 mwezi wa Desemba pekee na zaidi ya 80 kwa mwaka huu yameibua ghadhabu kwa wananchi wa Kenya.

Licha ya serikali kukanusha kuhusika, mashirika ya kutetea haki za binadamu, waathiriwa na wanaharakati wa vijana wanatoa wito kwa Wakenya kujiunga na maandamano hayo.

***BBC***

# Uhamiaji FC yapania usajili kufikia malengo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya kutofanya vizuri katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar, timu ya Uhamiaji FC, imesema lengo lake la kumaliza msimu huu ikiwa katika nafasi nne za juu bado lipo pale pale. Katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16, Uhamiaji FC ipo nafasi ya nane ikiwa imeshinda michezo sita, sare tano na imepoteza mechi nne.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa ,Walinzi wa Mipakani' hao, Mwinyi Hamadi, alisema hawahitaji kufanya makosa katika mzunguko wa lala salama kama ilivyokuwa katika mzunguko wa kwanza.

Alisema katika kuhakikisha wanafanikiwa kufikia lengo lao hilo, wataboresha kikosi chao kwa kufanya usajili wa nguvu katika kipindi hiki cha dirisha dogo.

**Hamadi alisema usajili wao huo umelenga kuchukua wachezaji kutoka klabu za Tanzania Bara na kwao visiwani Zanzibar.**

**Alibainisha kuwa wachezaji hao waliowalenga wanaendelea na mazungumzo na klabu zao ili kuona wanafanikiwa kuwanasa.**

**Alisema kwa mujibu wa mapendekezo ya benchi la ufundi la timu hiyo, katika ripoti yao ya nusu msimu wameomba kusajili katika nafasi ya ushambuliaji na mabeki.**

"Tutasajili wachezaji ambao wataleta mafanikio makubwa katika timu yetu, na uongozi utafanya usajili kwa mujibu wa mapendekezo ya mwalimu wa timu yetu," alisema.

Hata hivyo, alisema watahakikisha timu yao inafanya usajili mzuri na wakushtua katika kutoa burudani ya kiuchezaji uwanjani.

# KAGOMA AELEZEA UGUMU KWAKE KUIVAA SINGIDA BS

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Simba, Yusuph Kagoma, amesema ilikuwa ngumu sana kwake kucheza na wachezaji wa Singida Black Stars ambao anafahamiana nao.

Akizungumza baada ya mchezo wao dhidi ya Singida Black Stars, Jumamosi iliyopita ambao Simba ilishinda bao 1-0, Kagoma, alisema anafahamiana vizuri na wachezaji wa Singida Black Stars na alitegemea mchezo mgumu.

"Nimecheza nao muda mrefu, kwa hiyo tunafahamiana sana, nilifahamu mchezo utakuwa mgumu, lakini nashukuru nimetimiza majukumu yangu na timu kufanikiwa kupata ushindi," alisema Kagoma.

Aidha, alisema moja ya majukumu aliyopewa na kocha wake, Fadlu Davids, ni kuhakikisha anashika eneo la katikati na kuzuia mashambulizi ya wapinzani wao.

"Ila kocha anajua kama nimefanya kazi yake kwa usahihi kiasi gani, kikubwa tumepata ushindi na ndio lilikuwa lengo," alisema.

Kagoma, ambaye alisajiliwa na Simba akitokea klabu hiyo, alisema ligi inaenda mapumziko ikirejea wataendelea pale walipoishia.

"Ligi itasimama kwa muda, ni jambo zuri, bado tupo juu kwenye msimamo, ligi ikirejea tutaanzia hapa tulipoishia," alisema. Jumamosi Simba ikiwa Uwanja wa CCM Liti mkoani Singida, iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji wao, Singida Black Stars, ulioifanya kufikisha pointi 40 na kujihakikishia kula mwaka mpya ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, akiweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa viwanja vya michezo midogo midogo iitwayo Michezo kwa Maendeleo (Sports for Development), katika viwanja vya Mwera Regeza Mwendo Wilaya ya Magharib A, Unguja visiwani Zanzibar. Hafla hiyo fupi ilifanyika mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri asisitiza michezo kulinda afya

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wananchi kujihusisha na michezo mbalimbali ili kuimarisha afya zao kuepuka maradhi yasiyoambukiza.

Riziki alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akiweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa viwanja vya michezo midogo midogo iitwayo ,Michezo kwa Maendeleo' (Sports for Development) katika viwanja vya Mwera Regeza Mwendo Wilaya ya Magharibi A, Unguja visiwani Zanzibar.

Uwekaji huo wa jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa viwanja hivyo, ilikuwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo yanafikia kilele chake Januari 12, mwakani.

"Wataalamu wa afya wanahamasisha kufanya mazoezi au kujiingiza katika michezo mbalimbali, hivyo jiungeni na michezo kwani itasaidia kuimarisha afya na kujiepusha na maradhi yasiyoambukiza ikiwamo saratani, kisukari na shinikizo la damu," alisema Riziki.

Alisema michezo pia ni ajira na ni sehemu ya kukuza uchumi kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla hasa kwa vijana wa jinsia zote, kwa kuwa inawasaidia kujiepusha na vitendo viovu vinavyojitokeza katika jamii.

"Nitoe wito kwa wazazi na walezi kuwaruhusu mabinti zenu kushiriki katika michezo kwani si uhuni, cha muhimu ni kuzingatia nidhamu, maadili, mila na silka na utamaduni wa Kizanzibari," alisema.

Awali, mwakilishi wa Shirika la Kimataifa la Ujerumani GIZ, Lucy Moto, alisema mradi wa ujenzi wa viwanja vya michezo midogo midogo umelenga kujenga viwanja sita Zanzibar.

Alifafanua kuwa viwanja vitatu vitajengwa Unguja na vingine idadi kama hiyo kujengwa Pemba kwa ajili ya mpira wa kikapu, pete na wavu, na kwamba mradi huo utazingatia usawa wa kijinsia.

"Lengo ni kuondoa mila potofu kwa wanawake na wasichana kwani zinakwamisha maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa wanawake na hata kwa taifa," alisema Lucy.

## ZISIKUPITE

### ARNOLD NA LIVERPOOL

MLINZI wa kulia wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26, yuko mbioni kusaini mkataba na Real Madrid, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa England akiendelea kupuuza ofa mpya za kuongeza mkataba wake wa sasa unaomalizika msimu huu wa majira ya joto. ***(AS)***

### LIVERPOOL YAWINDA MABEKI

LIVERPOOL itawanunua beki wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong na wa Bayern Munich, Alphonso Davies, wote miaka 24, ikiwa Trent Alexander-Arnold atajiunga na kikosi cha Real Madrid. ***(Team talk)***

### AINA KUMRITHI WALKER

KLABU ya Manchester City inammfuatilia beki wa kulia wa Kimataifa Nigeria na Nottingham Forest, Ola Aina mwenye umri wa miaka 28, kama mbadala wa Kyle Walker, 34**.** ***(Sun)***

### RONALDO AIKATAA CITY

MSHAMBULIAJI wa Ureno na Al-Nassr, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 39, amekataa kuhamia Manchester City, licha ya kuwa amewachezea wapinzani wake, Manchester United kwa misimu miwili. (***Talksport)***

### KHUSANOV ANYATIWA

KLABU ya Newcastle United inavutiwa na beki wa kati wa Lens, Abdukodir Khusanov kwa pauni milioni 25, lakini wanakabiliwa na ushindani wa kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uzbekistan mwenye umri wa miaka 20, kutoka kwa timu za Ligi Kuu England, Manchester City, Tottenham Hotspur, Leicester City na Wolves. ***(Cronicle)***

### GRACIA AIVUTIA ARSENAL

ARSENAL inavutiwa na mlinda mlango wa Espanyol, Joan Garcia mwenye umri wa miaka 23, lakini klabu hiyo ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, imebakia ikisisitiza kuwa kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa raia huyo wa Hispania ni pauni milioni 25**.** ***(Mirror)***

### MITCHELL ATAKIWA ATLETICO

MLINZI wa kushoto wa Crystal Palace, Tyrick Mitchell mwenye umri wa miaka 25, hataki kuweka mustakabali wake wa muda mrefu katika klabu hiyo ya London, huku Atletico Madrid ikimtaka Mwingereza huyo. ***(Caught Offside)***

### ZUBIMENDI HAITAKI CITY

MANCHESTER City haina uwezekano wa kumfuatilia kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, ambaye bado hataki kuhamia England akitokea Real Sociedad. ***(TBR Football)***

### RUSHWORTH KUREJESHWA

KLABU ya Brighton inapanga kumrejesha tena katika kikosi chake, mlinda mlango, Carl Rushworth mwenye umri wa miaka 23, kutoka mkataba wa mkopo katika Klabu ya Hull City. ***(Football Insider)***

### KAMARA AGOMBEWA

SOUTHAMPTON na Ipswich zote zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Rennes na Finland, Glen Kamara mwenye umri wa miaka 29, katika dirisha la Januari. ***(TBR Football)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH: NIKO MBALI SANA KUSAINI MKATABA MPYA

●●●Kitu pekee katika akili yangu nataka Liverpool washinde ligi na ninataka kuwa sehemu ya...

**LONDON, England**

MOHAMED Salah amesema bado „niko mbali sana" kufikia muafaka wa mustakabali wake na Liverpool baada ya kufunga mara moja na kutengeneza mabao mawili kwenye ushindi wa 5-0 dhidi ya West Ham Jumapili, ambao uliifanya timu hiyo ya Kocha Arne Slot kuwa mbele kwa pointi nane kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England.

Salah mwenye umri wa miaka 32, anaweza kufungua mazungumzo na klabu nyingine kuanzia kesho, Jumatano (Januari Mosi, 2025) kuhusu uhamisho wa bila malipo kuelekea mwishoni mwa msimu, huku pale Liverpool mkataba wake wa sasa utamalizika Juni 30, 2025.

Wachezaji wenzake wa Liverpool, Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold pia wanaingia miezi sita ya mwisho ya mikataba yao hapo Anfield wiki hii.

Lakini licha ya sintofahamu inayoendelea kuhusu mkataba wake baada ya msimu huu, Salah alisema lengo lake ni kushinda taji akiwa na Liverpool na kwamba hayuko karibu kukubali mkataba mpya.

"Hapana tuko mbali na mkataba mpya," alisema Salah akiiambia Sky Sports.

"Kitu pekee katika akili yangu ni kuwa nataka Liverpool washinde ligi na ninataka kuwa sehemu ya hilo.

"Nitajitahidi kwa uwezo wangu wote ili timu ichukue kombe. Kuna timu zingine chache zitakutana nasi na tunatakiwa kuwa makini na kucheza kwa kujituma.

"Najaribu tu kufurahia mchezo. Mwisho wa siku nilikuja hapa kwa ajili ya matokeo na nilitaka kufanya kitu kwenye mchezo, lakini nina njaa zaidi ya mataji."

Kocha wa Liverpool, Arne Slot alisema hana wasiwasi kuhusu wachezaji hao watatu kuweza kufikia mazungumza, akisema kwamba anaamini bado anaweza kudhibiti hatima yao.

"Nadhani nina udhibiti mkubwa juu ya kile wanachofanya," alisema Slot.

„Kwenye uwanja wa mazoezi wapo pamoja na mimi, lakini wakizungumza juu ya maisha yao kibinafsi, hilo sina udhibiti nalo.

"Hivyo ndivyo hali ilivyokuwa mwaka mmoja uliopita, kumekuwa na hali kwa muda mrefu kama kocha, lakini nina uwezo wa kuwadhibiti kwa kiasi fulani kutokana na kile ninachotarajia kutoka kwao uwanjani na nimefurahishwa sana kuona Virgil analeta nini, Trent analeta nini na Mo analeta nini.

"Sasa jambo chanya kwangu ni kwamba kwa miezi minne au mitano ilikuwa Trent, Mo na Virgil tu, ambacho kilikuwa kinazungumzwa."

# Maguire ana imani kubwa na Amorim

**MANCHESTER, England**



MLINZI wa Manchester United, Harry Maguire, amesema staili na mbinu za Ruben Amorim ni "tofauti kabisa" na za kocha wa zamani, Erik Ten Hag.

Amorim aliteuliwa kuwa kocha wa Man United Novemba baada ya Ten Hag kutimuliwa kutokana na matokeo mabaya.

Baada ya mwanzo mzuri chini ya Amorim - kwa kushinda mara nne na sare katika michezo yake saba ya kwanza ikiwa ni pamoja na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya wapinzani wao, Manchester City - United wamepoteza mechi tatu mfululizo tangu Desemba 15.

Maguire aliiambia Sky Sports kwamba anatarajia kipindi cha mpito kitakuwa kigumu kwa timu hiyo kwani watamzoea kocha mpya.

"Jambo liko kwa makocha kwa mbinu na staili zao, kila mmoja ana mtindo tofauti," alisema Maguire.

"Nina uhakika mambo yatabadilika. Yeye (Amorim) anajua hasa anachohitaji kufanya ili kurudisha klabu hii kwenye njia yake.

"Ameingia na kufanya kila kitu anachohitaji kufanya. Anadai kweli."

United wameshuka hadi nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

# Sina hofu ya kufukuzwa Milan – Kocha

**MILAN, Italia**

KOCHA wa AC Milan, Paulo Fonseca, amepuuzia mbali uvumi kuhusu hatima yake, akisisitiza kwamba hajajadiliana na mtu yeyote na hana hofu.

Uvumi ulienea kwenye vyombo vya habari vya Italia kwamba anaweza kufukuzwa baada ya Milan kulazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani na AS Roma kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Timu yake haipo kwenye msimu mzuri hadi sasa, kwani ipo nafasi ya nane katika msimamo na ni ya 12 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Je, nilikuwa na mkutano mgumu na Zlatan?" alisema Fonseca kuhusu uvumi na kwamba alikutana na mshauri mkuu wa klabu hiyo na mchezaji wa zamani, Zlatan Ibrahimovic.

"Hapana, sijazungumza na mtu yeyote. Sijaona mtu yeyote kutoka kwenye uongozi. Siwezi kusema chochote zaidi. Siwezi kurekebisha mambo ambayo hayajafanyika," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Sijawahi na sina hofu maishani mwangu. Na nitaendelea hivi. Kwangu mimi ni muhimu kuwa na dhamiri safi kila wakati: Ninafanya kazi, ni mwaminifu kwa wale wanaofanya kazi nami.

"Siogopi chochote."

Fonseca alisema amepanga kuiongoza Milan katika nusu fainali ya Supercoppa Italiana baada ya mwaka mpya dhidi ya Juventus mjini Riyadh nchini Saudi Arabia.

"Naweza kutarajia," alisema. "Sina dalili za kinyume. Sasa narudi nyumbani, nitatazama mchezo, kisha nitafikiria kufanya kazi."

Alisema hajutii kazi aliyoifanya hadi sasa akiwa Milan tangu awasili Juni, akichukua mikoba ya Stefano Pioli.



# GUARDIOLA SASA AITOA CITY MBIO ZA UBINGWA

**LEICESTER CITY, England**

PEP Guardiola amesisitiza kwamba, Manchester City "haina nafasi" ya kushinda taji la Ligi Kuu England licha ya "ahueni" baada ya ushindi uliosubiriwa kwa muda mrefu dhidi ya Leicester City Jumapili.

City walicheza mechi tano mfululizo bila kushinda katika mashindano yote, lakini ushindi wa mabao 2-0 katika uwanja wa King Power, uliwapa ahueni huku wenyeji wakiwa wamejiweka kwenye hatari ya kushuka daraja.

"Si ya kufurahisha kwa sasa, ni ahueni tu," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports baada ya mchezo huo. "Tumefanya mazuri kwa miaka mingi."

Wakati matokeo hayo yameifanya City kujivuta hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

"Hatuwezi kudumu kwa dakika 90, leo (juzi), tumethibitisha hilo tena," alisema kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, akiiambia BBC Sport.

"Tunaweza kusafisha akili zetu sasa kwa kupata matokeo. Tuko mbali sana na kushinda Ligi Kuu. Tunakubali tayari hakuna nafasi ya hilo, lakini tuna mambo mengine ya kupigania. Kombe la FA, nne-bora na michezo ya kushinda inasaidia. "

Leicester ya Ruud van Nistelrooy imebakia nafasi ya 18 baada ya mabao ya Savinho na Erling Haaland katika mchezo wa 500 wa Guardiola akiwa kocha wa Man City.

"Walikuwa bora kuliko sisi katika kipindi cha pili," aliongeza Guardiola.

"Huu ni mchezo mmoja tu, mchezo dhidi ya Manchester United ulituumiza sana katika hali ya kujiamini, mchezo ule ulituua, mchezo huo ulikuwa wa kusuasua kiakili kisha mechi ngumu dhidi ya Aston Villa na Everton.

"Ndivyo ilivyo, tunapaswa kuwinda ushindi na hayo ndiyo maisha. Wachezaji wengi walithibitisha tena kuwa wako tayari kupigana."

City wana mapumziko ya siku sita kabla ya kuwakaribisha West Ham baada ya mwaka mpya.

# NYOTA 28 WAITWA KUUNDA KIKOSI CHA KILIMANJARO STARS

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya wachezaji 28 wameitwa kwenda kuunda kikosi cha Timu ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars, kitakachoshiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi inayotarajiwa kuanza Januari 3, mwakani, kwenye Uwanja wa New Amaan, Zanzibar.

Kikosi hicho kitakuwa chini ya Ahmad Ally, ambaye naye kwa mara ya kwanza, ameteuliwa kuwa Kocha Mkuu wa kikosi hicho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo ambaye ni Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, alisema amepata furaha isiyo kifani kwani hajawahi kuifundisha timu yoyote ya taifa kwenye historia yake kisoka.

Alisema kuteuliwa kwake kunaonesha imani kubwa kwake, ambapo kupitia kikosi hicho ataendelea kujifunza, lakini pia atakuwa ametengeneza wasifu mkubwa kwani ni ndoto ya kila mwalimu kuifundisha timu ya taifa.

"Kusema kweli mimi binafsi sikutarajia hili kwa wakati huu, imekuwa ni ‚sapraizi', jana (juzi), ndiyo nipewa taarifa rasmi ya kukifundisha kikosi hicho, baada ya hapo tukakaa na Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), kutengeneza kikosi hiki, na tuliangalia malengo ambayo ni kutengeneza uwezo wa vijana ambao watakwenda kucheza AFCON 2027 na kuchukua wachezaji wa timu ya taifa ambao hawapati nafasi mara kwa mara ya kucheza ili nao waweze kupata nafasi kwenye michuano hii ya Mapinduzi kwani huko mbele tuna michuano ya CHAN pamoja na AFCON 2027," alisema kocha huyo.

Walioitwa kuunda kikosi hicho, ni Metacha Mnata na Ayoub Lyanga wa Singida Black Stars, Ramadhani Chalamanda, Said Naushad na Hijja Shamte kutoka Kagera Sugar, Antony Mpemba, Lusajo Mwaikenda, Paschal Msindo, Sospeter Bajana, Abdulkarim Kiswanya, Idd Selemani ‚Nado', Nassor Saadun, na Abdul Hamisi Sopu, wote kutoka Azam FC.

Wengine ni Nickson Mosha na Ahmed Pipino wa KMC, Vedatus Masinde kutoka TMA, Lameck Lawi, Semfuko Charles na Bakari Msimu wote wakitokea Klabu ya Coastal Union, Wilson Nangu, Gamba Idd na David Brayson wa JKT Tanzania.

Wachezaji wengine walioitwa ni Zidane Sereri wa Dodoma Jiji, William Edgar wa Fountain Gate, Offen Chikola kutoka Tabora United, Joshua Ibrahim wa KenGold, Sabri Kondo wa KVZ na Crispin Ngushi kutoka Mashujaa FC.



Waendesha baiskeli wanane kutoka Nairobi wakiwa pamoja baada ya kufika mkoani Kilimanjaro kukabidhi mabegi kwa Shule ya Msingi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. **MPIGAPICHA WETU**

# Waendesha baiskeli kwa siku 4 kutoka Nairobi hadi Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu**

WAENDESHA baiskeli nane kutoka Naironi nchini Kenya, wametumia siku nne kufika mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kukabidhi wanafunzi mabegi maalum ya shule yaliyotengenezwa kwa plastiki.

Mabegi hayo yamegawiwa kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro mkoani humo.

Akizungumza wakati wa kuwapokea waendesha baiskeli hao pamoja na kugawa mabegi hayo, Meneja wa KLM kwa upande wa Tanzania, Rajat Kumar, alisema mpango huo wa kutengeneza mabegi ya plastiki ni mkakati wao wa kutunza mazingira.

Alisema mabegi hayo yametengenezwa kutokana na chupa za plastiki zilizotumika kwenye ndege za shirika hilo.

"Waendesha baiskeli hawa ambao wametumia siku nne kutoka Nairobi kuja Kilimanjaro wanaungana na jamii nyingine katika mkakati wa kutunza mazingira kama tunavyopambania KLM," alisema Kumar.

Alisema Tanzania ni nchi ya pili kupokea mabegi hayo kwa nchi za Afrika na kwamba ya kwanza ilikuwa Kenya ambapo mabegi hayo yalipokewa kwa shule ya Msingi Muthangari jijini Nairobi, Februari mwaka huu.

Waendesha baiskeli hao wanatarajia kuanza safari ya kurejea Nairobi baada ya kufanikisha safari hiyo maalum.

## Ramovic apagawa viwango Yanga SC

INATOKA UK. 24

ufundi muda mfupi tu baada ya mchezo kumalizika, alisema ubora wa wachezaji ndiyo ulioamua mechi. "Ugumu wa mechi ulikuja kutokana na ubora wa wachezaji, uwekezaji wa Yanga ni tofauti na timu yetu, makosa yaliyofanyika kwa wachezaji wangu ni kwa sababu hiyo tu ya uwekezaji wao mzuri umeamua mechi ya leo," alisema Muya.

Kocha huyo akafichua kuwa kuna baadhi ya wachezaji ambao walikuwa kipaumbele kwenye usajili kabla ya kuanza kwa ligi, lakini hadi leo hii hawajacheza kwa kukosa vibali, wengine kukosa leseni za usajili.

Fountain Gate imebaki nafasi ya sita, ikisalia na pointi zake 20, ikicheza michezo 16, kushinda sita, sare mbili na kupoteza minane, mabao 24 ya kufunga, kufungwa mabao 32, ikiongoza kwa kuruhusu mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

## Fadlu aanika nafasi tatu za kusajili Simba

INATOKA UK. 24

kufunga, ikiruhusu matano.

Akizungumzia michuano ya Kombe la Shirikisho, alisema kundi lao bado ni gumu na kwamba katika makundi yote ndilo unaweza ukaliita la kifo.

"Ninachoweza kusema kundi letu unaweza kuliita kundi la kifo kwa kuwa kila timu ina nafasi ya kufanya kitu tofauti, timu mbili zinatakiwa kusonga mbele, lakini kuna timu tatu au hata nne zina nafasi hiyo, sisi Simba tunatakiwa kuwa na hesabu kubwa kwenye hizi mechi mbili za ugenini na moja ya nyumbani," alisema.

Hata hivyo, alisema wachezaji wake wanatakiwa kubadilika na kutofanya makosa kama waliyoyafanya nchini Algeria walipocheza dhidi ya CS Constantine, akisema ilikuwa ni mechi ya kuondoka na pointi zote tatu, au japo moja, lakini wakapoteza kwa mabao 2-1 kutokana na makosa yao, lakini kwa sasa wamejifunza kutokana makosa hayo.

Kuhusu Elie Mpanzu, winga aliyeanza kuitumikia timu hiyo kipindi cha usajili wa dirisha dogo, alisema yeye binafsi anafurahishwa na kiwango chake ingawa anajua shauku ya mashabiki ni kumuona anafunga mabao au anatengeneza.


"Nimefurahishwa sana na kiwango chake, najua shauku ya mashabiki wa timu hii ni kumuona anafunga bao au anatoa ‚asisti', lakini kwangu naona anafanya makubwa uwanjani.

"Mimi kama kocha nawaambia wanachama na mashabiki wa Simba, pamoja na wapenzi wa soka watulie hivyo hivyo, atawashangaza sana, kwa sababu nimeshamuona ni mchezaji wa kiwango cha juu sana," alisema Fadlu.

Michezo
Jumanne Desemba 31, 2024
Nipashe

## Salah: Niko mbali sana kusaini mkataba mpya

UKURASA 21



MKONO...




Kiungo mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, akimpongeza mshambuliaji mwenzake, Diogo Jota, kwa kupachika bao la tano dhidi ya West Ham United wakati wakishinda 5-0, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa London juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# FADLU AANIKA NAFASI TATU ZA KUSAJILI SIMBA

Kujifungia na mabosi, huku akisema zinahitajika hesabu kali mechi mbili za ugenini michuano CAF ili...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, anatarajia kwenda kukaa na viongozi wa klabu hiyo kuangalia nini kifanyike kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chake.

Akizungumzia tathmini ya kikosi cha timu hiyo baada ya kumalizika kwa michezo 15 ya mzunguko wa kwanza, pamoja na mechi za Kombe la Shirikisho Afrika, kocha huyo raia wa Afrika Kusini, alisema anataka kukaa nao ili waangalie ni mchezaji gani bora anaweza kupatikana kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili wapate kumwongeza kwenye kikosi.

Alisisitiza kuwa hahitaji kuongeza mradi tu ionekana amesajili bali anataka mchezaji ambaye atakuja moja kwa moja kuchukua nafasi au kuleta ushindani mkubwa kwenye kikosi.

"Nakwenda kukaa na viongozi kuangalia nini kifanyike, nani anapatikana sokoni ili tumwongeze, kazi bado ni kubwa, nyuma, katikati na mbele kote kunahitaji maboresho angalau ya mchezaji mmoja mmoja, ukiangalia ushindani kwenye Ligi Kuu ni mkubwa, kuna Azam FC, Singida Black Stars, Tabora United na Yanga pamoja na sisi wote tuna uwezo wa kuchukua ubingwa, hivyo lazima tuendelee kuongeza uimara kwenye kikosi chetu," alisema kocha huyo.

Simba imemaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ikiwa kileleni, ikikusanya pointi 40, ikicheza michezo 15, ikishinda 13, sare moja, ikipoteza moja, mabao 31 ya

INAENDELEA UK. 23

## Ramovic apagawa viwango Yanga SC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amewavulia kofia wachezaji wake akisema kiwango walichoonesha kwenye mchezo dhidi ya Fountain Gate, kimeonekana kumshangaza hata yeye mwenyewe.

Ramovic, ambaye aliiongoza Yanga kuifumua Fountain Gate mabao 5-0 katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi katika Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, alisema wakati mwingine anaangalia wanavyocheza haamini kile anachokiona, kwani walionekana kuwa na kiwango bora zaidi kuliko alivyotegemea.

"Napenda kuwapa pongezi wenzangu wote, hasa watu wa eneo la utimamu wa mwili, wamefanya kazi kubwa hadi kufika leo hapa, si kazi rahisi kuifunga kila timu tunayokutana nayo kwenye ligi kwa idadi hii ya mabao, kwani nyingi zinakuja kupaki basi, zinacheza nyuma ya mpira na kujaribu kutushambulia kwa kushtukiza, ni ngumu, lakini wachezaji wangu wameweza kufanya kazi kubwa kiasi cha kunishangaza hata mimi, wakati mwingine siamini nini wanakifanya mle uwanjani, ni jambo la kujivunia sana," alisema kocha huyo.

Kocha huyo bado anaamini kuwa wachezaji wake hawajafikia kiwango cha utimamu wa mwili ambacho yeye anahitaji wawe nao, lakini akaongeza hawapo mbali na hilo.

"Napenda mpira wa kasi, kushambulia muda wote wa mchezo, huwa inahitaji pumzi na fiziki, bado hatujakuwa fiti kwa asilimia 100, lakini tunakwenda kwenye njia sahihi tuliyoipanga," alisema.

Alitahadharisha kuwa iwapo watafika kwenye kiwango anachohitaji anadhani kikosi kitakuwa ni hatari zaidi ya kilivyo sasa.

Kocha huyo ameiongoza Yanga kushinda michezo mitano mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, akianzia dhidi ya Namungo FC, ikishinda mabao 2-0, mabao 3-2 dhidi ya Mashujaa FC, 4-0 dhidi ya Prisons na Dodoma Jiji, kabla ya juzi kupata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Fountain Gate.

Imefikisha pointi 39, ikiwa nafasi ya pili nyuma ya Simba inayoongoza ligi ikiwa na pointi 40, huku zote zikiwa zimemaliza rasmi mechi zao15 za mzunguko wa kwanza.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, ambaye alitimuliwa kazi yeye na benchi lake lote la

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002